Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

# Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

**Nukuu ya Qur'an Tukufu**

**Yeye Ndiye Aliyelifanya jua kuwa mwanga na mwezi kuwa wenye nuru, na Akaukadiria vituo ili mjue idadi ya miaka na hesabu. Allah Hakuviumba hivyo ila kwa haki. Huzieleza Ishara kwa watu wanaojua.**
***(Sura Yuunus 10:6).***

JUZU 75 No. 182 | RAB. 1/ RAB. 2. 1436 AH | JANUARI 2015 | SULHU 1394 HS | BEI TSH. 500/=

## Khalifa mtukufu aombea kheri ya mwaka 2015 na kusema:

# Mabadiliko ya tarehe yataleta maana tu iwapo tutayatumia kujitathmini

*Na Mwandishi wetu:*

Katika hotuba yake ya Ijumaa ya kwanza ya mwaka 2015, Kiongozi mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya duniani, Khalifatul Masih V, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a., baada ya Tashahhud, Taaudh na kusoma Suratul Faatiha, alisema:

Leo ni Ijumaa ya kwanza ya mwaka 2015 na Hazrat Masih Khalifatul alisema kwamba alipokea salamu kutoka kwa watu mbalimbali kwa njia ya mtu binafsi na kupitia nukushi wakimtakia heri ya Mwaka Mpya naye mwenyewe alituma salamu zake kwa kila mtu.

Salamu za kutakiana kheri ya Mwaka Mpya zitakuwa tu na maana wakati sisi kutafakari na kuona ni kiasi gani hasa tumetekeleza majukumu yetu ya kuwa Waahmadia mwaka jana na ni kwa kiasi gani pia tutajaribu kufanya hivyo katika mwaka huu. Kuanzia Ijumaa hii na kuendelea tunapaswa kufanya maazimio ambayo yatatupelekea kujenga umakini na juhudi katika Mwaka Mpya. Ni dhahiri kwamba kazi ambazo tunatarajiwa kuzifanya kama Waahmadiya zinaweza tu kufanyika kwa njia ya fadhila ya ucha Mungu. Hata hivyo, swali ni hili kwamba ni kipi kinatakiwa kiwe kiwango chetu cha ucha Mungu na

*Endelea uk. 3*

# Mahafali ya Kihistoria - 2014 Shule ya Sekondari Ahmadiyya

## • *Amir sahib atunuku zawadi na kuahidi maendeleo zaidi*

**Na Mwandishi wetu**
**Dar es Salaam**

**"Walikuwepo wazee kama Walikuwepo wazee kama Salum Kungulilo, Iddi Ramadhani, Ally Salum Ndendekile, Musa kiwanga, Mzee Msabaha n.k ambao waliomba usiku na mchana ili jumuiya iwe na shule yake, lakini hawakubahatika kushuhudia tunu hii ambayo leo sisi tunaishuhudia".**

Maneno haya yalisemwa na mmoja kati ya viongozi waliopata fursa ya kueleza machache katika Mahafali ya kuwaaga wanafunzi ambao wamehitimu kidato cha nne katika Shule ya Ahmadiyya Secondary School- Kitonga. Haya ni mahafali ya kwanza yaliyofanyika tarehe 16.11.2014 katika eneo la Jumuiya ya Ahmadiyya ambapo ndipo ilipo shule hiyo huko Kitonga, nje kidogo ya jiji la Dar es salaam.



*Amir Sahib Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akiwa kwenye picha ya pamoja na wahitimu wa kidato cha Nne 2014 kwenye Shule ya Sekondari ya Ahmadiyya pamoja na watendaji wengine wa Shule katika siku ya mahafali*

Mwenyekiti wa hafla hiyo ambaye pia ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Shule Mwl Abdulrahman Ame, aliifungua hafla hiyo sawa na ada ya Islam kuwa lisianze jambo bila ya maombi. Na hakuna maombi makubwa mbele ya Allah baidi ya kuran Tukufu, ambayo ilisomwa na mwanafunzi kutoka shuleni hapo Fadhilillah A.Ame. Alisoma sura 31:13-20. Ikufuatiwa na wimbo wa Taifa ulioimbwa na wanafunzi kwa watu wote kusimama kwa heshima, na baadae ukafuatia wimbo "Tanzania Tanzania , nakupenda kwa moyo wote". wimbo ambao, mrindimo wa sauti na maudhui yaliyo ndani ya wimbo huo, humtoa vipele vya msisimko mwilini na hata machozi yeyote avutaye fikra miaka ile ya sabani na themani, wakati ambapo Umoja wa kitaifa ulikuwa si jambo la kutafutwa kwa Kurunzi. Hakika wimbo huo uliakisi hasa hadithi ya Mtukufu Mtume Muhammad S.a.w kuwa "kuipenda nchi yako ni sehemu ya Imani". Baada ya wimbo huo ikafuatia shairi la Masihi aliyeahidiwa lililosomwa na Mwalimu Muhsin Abas Kaye.

Mtu wa kwanza kupewa fursa ya kuongea alikuwa ni Mwl Badru Musoke.huyu alikuwa Mkuu wa shule wa kwanza katika shule hii. Yeye alieleza historia kwa ufupi pindi shule ilipoanzishwa. Hamasa waliyokuwa nayo pamoja na changamoto walizo kumbana nazo. Alisema shule ilianza tarehe 17 januari 2010 ikiwa na wanafunzi 7 tu, hadi temu ya kwanza inamalizika tulikuwa na wanafunzi 23.baadhi ya wanafunzi walikuwa ni

*Endelea uk. 2*

# Mapenzi ya Mungu

## Maoni ya Mhariri

# WAHESHIMIWE

**Waafrika kwa ujumla wao walilaani na kukataa kwa nguvu zao zote kutawaliwa. Kwao hali hiyo ilikuwa ya huzuni na fedheha na kadri ya uwezo wao walipambana kulinda heshima na utu wao. Walifika hata hatua ya kuwa tayari kumwaga damu.**

**Tunayo majina ya viongozi ambao wakishirikiana na watu wao walipigana kufa na kupona ili kulinda uhuru wa jamii zao. Viongozi hao waliona ya kwamba ndege siku zote haoni raha anapowekwa tunduni, hata tundu hilo liwe la dhahabu. Mmwagie chakula cha aina yoyote ile bado atakuwa na manung'uniko moyoni na atafurahia kwenda kula pumba na vitu vingine vya hovyo kuliko kuwa katika tundu la dhahabu na kula vinono. Ndege anahitaji fursa, wasaa aruke na arande na huku akiangalia chini na kufurahi. Viongozi wa namna hii wanaoheshimu uhuru ni wengi katika historia ya Afrika. Samora Toure, Robengura, Mkwawa kwa kuwataja wachache tu.**

**Viongozi hawa walipanda mbegu ya hasira ambayo ilitusaidia sana katika mapambano yetu ya kupata uhuru katika Afrika. Kwa kweli kilikuwa ni kipindi kigumu na kilichohitaji kujitolea kwa hali na mali. Viongozi wetu hao mashujaa walijitolea kwa kila kitu. Walikuwa tayari kwenda jela, walikuwa tayari kufunga saumu, walikuwa tayari kupigwa na kupewa manyanyaso ya kila aina hayo yote hayakuwafanya wasahau shabaha na dhamira ya kuwa huru.**

**Mapambano hayo yalifanikiwa na Afrika ikakombolewa. Ni dhahiri ya kwamba tuliendelea kuwaheshimu sana viongozi hao na kuwapa nafasi ya pekee katika nyoyo zetu. Lakini kwa bahati mbaya tukawa tumesahau methali ile kwamba; 'ukimsifu mgema, tembo huliweka maji'. Viognozi hao tuliowapenda wakalewa na wakaanza kutangaza juu ya umuhimu wa fikra zao wakisisitiza kwamba 'zidumu fikra za mwenyekiti'. Wengine wakasahau kwamba kuna siku wataonja m auti, wakatangaza kwamba wao ni marais wa m ilele. Uhuru wa kuzungumza ukafinywa, uhuru wa mawazo ukabanwa, ilimuradi fikra zinazotawala nchi zikabaki kuwa ni fikra za mtu mmoja tu.**

**Tulikwenda mbali mpaka watu wakaanza kufikiria ya kwamba kiongozi huyo anajua kila kitu, kwamba kiongozi huyo hakosei, kwamba fikra zake zote ni sahihi, wakamtoa katika hali ya ubinadamu na kumvisha koti ambalo halikuwa m akamo yake.**

**Ni katika ulevi huo wa kufikia hatua (Mwenyezi Mungu Apishe mbali) ya kuwaabudu viongozi ndipo ikatoka sauti kutoka katika mji wa kale Mombasa sauti ya Al-Amini Al-Mazrui Profesa wa masuala ya Siasa na akaandika na kutangaza ya kwamba; "Ni vizuri sana kuwaheshimu na kuwaenzi viongozi wetu, lakini tunakosea mno tukifika kwenye hatua ya kuanza kuwaabudu". Hili alilipinga kwa nguvu zake zote na kifo chake katika mwanzo wa Mwezi huu kinatukumbusha ya kwamba fikra huendelea kuishi na kinachokufa ni mwili tu. Tunadhani tunaweza kukumbuka kifo cha Profesa Ali Al-Amini Mazrui kwa kuyazingatia maneno hayo ya busara aliyoyatoa ili kuwaonya viongozi ambao licha ya kazi nzuri waliyoifanya hapo mwanzoni wameitia hasara kubwa Afrika. Afrika hivi leo ni maskini sana ingawaje ni tajiri sana. Afrika hivi leo imekumbwa na maradhi yote unayoweza kuyafikiria. Afrika leo ina maradhi ya ukabila, magomvi ya dini, kugombea mipaka na wale walio madarakani kutokuwa na ndoto hata kidogo ya kuachia ngazi.**

**Tunadhani wakati umefika wa Afrika nasi kutambua ya kwamba uongozi ni babu amana na kwamba inatakiwa siku zote tuelewe ya kwamba tukisha timiza wajibu wetu sawa na makubaliano yetu ya katiba kiongozi anatakiwa kwa hiyari bila ya kupitisha mbinu na mikakati ili gurudumu la nchi liweze kwenda katika mikono ya viongozi wengine. Ni utamaduni huu ambao Profesa Ali Mazrui aliupigania na utamaduni huo unaoweza kuleta ukombozi wa kweli kwa Afrika. Mungu ibariki Afrika.**

# Mahafali ya Kihistoria - 2014

*Kutoka uk. 1*

changamoto kubwa kwetu. vijana tulioanza nao wengi wao walikuwa wameisha kata tamaa ya kusoma kabisa. Na kuna baadhi tuliwapokea hali yao ya kimasomo ilikuwa iko chini sana, lakini tuliwachukua na kupambana na changamoto zao na hatimae katika mtihani wa taifa wa kidato cha pili wakaweza. Hivyo tunawaombea sana , ili matokeo yao ya kidato cha nne yawe matokeo bora sana ili waendelee na masomo na pia iwe ni njia ya kuitangaza shule yetu. Akiwanasihi wanafunzi wanao hitimu alisema, ninawaomba nyie ambao mmemaliza na kusubiri matokeo yenu, msikae bila kazi yoyote bali jitoleeni kufanya kazi za jamaat.kwani jumuiya inazo kazi nyingi mno, hapa makao makuu na hata mikoani. Lakini pia wapo wadogo zenu ambao wanahitaji msaada wenu wa kitaaluma, muwafundishe yale mnayo yajua. Mwisho alitoa shukrani za dhati kwa ushirikiano na msaada aliupata kutoka kwa Huzoor atba, Amir Sahib, Kamati ya shule, wanajumuiya na walimu wenzake ambao walifanyakazi kama wendawazimu bila kuchoka.

Aliefuatia alikuwa ni Mwenyekiti wa kamati ya shule, Mwl Abdulrahman Ame ambaye nae alielezea kwa muhtasari haja, sababu na malengo ya Jumuiyya kuanzisha shule. Alisema historia ya shule hii inaanzia mbali sana hususan wazo hili lilikuwepo tangu inasajiliwa Jamaat yetu miaka ya 1930. Viongozi na wazee wetu walikuwa na mawazo ya kuwa na shule. Hivyo miaka hiyo ya mwanzoni walianzisha shule ya msingi katika eneo la pangale huko Mkoani Tabora, lakini kwa bahati mbaya ilitaifishwa na serikali. Lengo la Jamaat kuwa na shule ni kwamba, pamoja na wanajamaat kupata masomo ya (secular) pia iweze kuwafinyanga vijana weke katika khulka, mwenendo bora, maadili mazuri. Hivyo kwa fadhila za Allah, mwaka 2010 Amir wa Jumuiya wa wakati huo Mzee Ali Saidi Mose aliwaita baadhi ya wanajumuiya akiwemo katibu wa Jumuiya wa wakati huo yeye mwl Ame, Mzee Mahmud Khamsini Mubiru , Mzee Sultani Ungando na wanajamati wengine akawakumbusha wazo hili la kuwa na shule. Katika kikao kile Mzee sultan Ungando akaahidi kutoa eneo lake takriban heka moja lililoko eneo la kitonga kwa ajili ya mpango huo. Baada ya kupatikana eneo, Jamaat ikaongeza kununua eneo lingine la heka kumi na moja. Ikaundwa kamati ya ujenzi na usimamizi wa



*Baadhi ya wasichana waliohitimu kidato cha Nne 2014 kwenye Shule ya Sekondari ya Ahmadiyya wakisikiliza kwa makini hotuba ya Amir na Mbashiri Mkuu aliyoitoa kwenye mahafali hayo. mahafali*

shule na hatimae hamasa ya kuchangia ujenzi ikaanza na mwaka huo 2010 darasa moja likajengwa na 2011 tarehe 17 januari shule ikaanza rasmi. Changamoto zilikuwa nyingi sana ikiwemo madarasa na mabweni, lakini tulikabiliana nazo sawa na Mwenyezi Mungu Alivyotuwezesha . Hatimae tulifanya mtihani wa taifa wa kidato cha pili shule ya jirani maana usajili hatukuwa nao. Alhamdulillahi matokeo yalitupa nafasi ya 88 kati ya shule 303 kwa mkoa wa Dar es salaam hivyo yalitupa hamasa sana. Aliendelea kusema kuwa, shule hivi sasa imepata usajili kutoka

Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi kwa namba ya usajili **4681,** na pia imesajiliwa kama kituo cha kufanyia mitihani na Baraza la Mitihani ya Taifa kwa namba ya usajili **5081**. Shule ina jumla ya wanafunzi 125 kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne.

Mkuu wa shule anayeongoza hivi sasa Mzee Mahmud Khamsin Mubiru akielezea uanzishwaji wa shule, changmoto na maendeleo yake, pia aliwaomba wadau mbalimbali wa shule hii waliohudhuria pale na wale walio mbali kuwa, kwa wale ambao walibahatika kwenda shule na wanavyo vitabu majumbani mwao wavilete ili kuboresha maktaba ya shule. Pia alisema, Elimu haina mwisho. Hivyo ni vema mmiliki na wadau wa shule hii waangalie uwezekano wa kuwa na kidato cha tano na sita angalau kuanza na mikondo isiyo ya sayansi.

Mwl Mohamed Ngunde ambae ni mwalimu wa Taaluma, akiwasilisha taarifa yake ya miaka mine alisema, Shule hii ni ya kutwa na bweni yenye jumla ya masomo 12 yakiwemo masomo ya sayansi, sanaa, dini na biashara. Maaendeleo kitaaluma yanapimwa kwa ufaulu wa wanafunzi. Akieleza mafanikio hayo mwalimu alisema, katika mtihani wa Taifa wa kidato cha pili 2012, shule yetu ilifanya mtihani huo kwa mara ya kwanza. Matokeo ya mtihani huo, shule ilishika nafasi ya 88 kati ya shule 303 za mkoa wa Dar es salaam. Mtihani kama huo pia ulifanywa 2013 na shule yetu ikashika nafasi ya 81 kati ya shule 304 za mkoa wa Dar es salaam.

Akiwaasa wanafunzi waliohitimu kidato cha nne mwalimu Ngunde aliwataka waitumie taaluma waliyoipata katika kipindi chote cha miaka 4 ili iweze kuwa ni chanzo cha mafanikio yao, wazazi , Jamaat pamoja na nchi kwa ujumla.

Kuporomoka kwa maadili katika nchi na duniani kwa ujumla ni miongoni mwa sababu za kuanzishwa kwa shule hii ya Ahmadiyya. Hivyo, malengo yetu sasa ni kutoa elimu bora, malezi bora na nidhamu bora kwa Wanajamaat na jamii kwa ujumla. Pia kuwasaidia WaAhmadiyya na jamii kupata elimu kwa urahisi kwa ulipaji wa ada ya shule kidogo kidogo sawa na sera ya Jamaat kutoa huduma na kuwasaidia wazazi ambao uwezo wao ni mdogo kuwapeleka wana wao katika shule bora nchini. Haya yalisemwa na Meneja wa shule bw Musa Mgeleka katika mahafali hayo.

Bw, Mgeleka alisema; Ada ya

***Endelea uk. 5***

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

# Khalifa mtukufu aombea kheri ya mwaka 2015:

*Kutoka uk. 1*

wema! Ni lazima kuwa wazi kwa kila mtu anayejiunga na Ahmadiya au ambaye tayari yu Mwahmadiya kwamba Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) alibainisha daraja/viwango hivi kwa ajili yetu. Na sasa kwa rasilimali zote na teknolojia ya kutosha iliyopo duniani kila Ahmadia anachukua ahadi angalau mara moja kwa mwaka kwa Khalifa wa zama ya kufanya juhudi yake ipasavyo ya kufikia viwango vya wema na uchamungu kama ilivyoelezwa na Masihi Aliyeahidiwa (a.s).

Hakika kiwango kinachotarajiwa kwa Ahmadiya kimeelezwa katika ahadi ya Bai'at. Ingawa ahadi za Bai'at ni kumi, hata hivyo, kwa upana wa maneno (zifafanuliwapo) zinabeba majukumu zaidi ya thelathini juu ya Ahmadiyya. Kama tunataka tupate furaha ya kweli ya kuadhimisha Mwaka Mpya hatuna budi kuyatia majukumu haya maanani. Haitoshi kuwa na furaha kwa sababu tu ya kukubali suala la kifo cha Yesu / Nabii Issa a.s au kwa kuwa tumemkubali yule ambaye alikuwa ameahidiwa kuja katika zama hizi. Bila shaka hiyo ni hatua ya kwanza na muhimu lakini Masihi Aliyeahidiwa a.s alikuwa na matarajio makubwa juu

yetu kuwa tutaelewa kwa kina juu ya wema na ucha Mungu na kufanya mazoezi ya kuufikia. Na kwamba tutajitahidi kuepukana na dhambi kama vile mmoja wetu anavyojilinda dhidi ya mdudu anayenyonya damu. Kisha si hivyo tu bali sisi tunatakiwa tuwe na uwezo wa kuleta mabadiliko ya kimapinduzi ndani yetu wenyewe na pia kuwa chanzo cha mabadiliko ya dunia na kuileta dunia karibu na Mungu. Maelezo juu ya jambo hili yanahitajika kuelezwa mara kwa mara na bila shaka kukumbusha huku kwa kurejewa rejewa ni jambo muhimu sana.

Ahadi ya kwanza ambayo sisi tumefanya [katika masharti ya Bai'at] ni kuepukana na shirk (kumfanyia washirika Mwenyezi Mungu). Wakati muumini wa kweli anamuamini Mwenyezi Mungu na kutokana na imani hiyo pia anampokea Imamu wa zama, yeye sasa hatakiwi awe na hata alama ya mbali ya kumshirikisha Mwenyezi Mungu na kitu chochote. Shirk ilivyoelezwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s si ile tu ya ibada ya masanamu kwa dhahiri.

Badala yake inahusu hasa shirk iliyofichikana ambayo inadhoofisha imani ya muumini. Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alisema kuwa: Kuamini Umoja wa Mungu hakuna maana tu kutamka kwa maneno ya kukiri kwamba hapana anayestahili kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu lakini mtu akawa na maelfu ya mawazo ya kishirikina moyoni mwake. Mtu ambaye anatoa kipaumbele au umuhimu zaidi kwa kazi yake yoyote au mipango yake yoyote, au juhudi zake zozote na kuzitegemea sawa na ambavyo Mwenyezi Mungu apaswa kutegemewa au anatoa umuhimu mzito kwa nafsi yake mwenyewe kuliko anavyotoa umuhimu juu ya Mwenyezi Mungu, mtu huyo yu mshirikina mbele ya macho ya Mungu katika matukio yote haya. Sanamu si kinyago tu cha dhahabu, au cha fedha, au shaba au jiwe ambavyo vinategemewa na wachongaji wake. Kwa kweli kila kitu, kila neno, kila mipango ambayo huhesabiwa na kupewa ukuu na umuhimu ambao unastahili kupewa Mungu ni sanamu katika macho ya Mwenyezi Mungu.

Tunahitaji basi kujitathimini leo iwapo tulivichukulia vitu vya kidunia kuwa ndio kila kitu katika mwaka uliopita au tulivitumia tu kwa ajili ya kupangia mipango na kisha tukategemea wema na baraka zote kutoka kwa Mungu. Tafakuri ya kina isiyo na ubinafsi ya kujitathmini sisi wenyewe itatupatia jawabu.

Kisha Masihi Aliyeahidiwa a.s. alichukua ahadi yetu kwamba tutajitenga mballi kabisa na uongo. Ni mtu gani aliye na akili zake anayeweza kusema kwamba uongo ni jambo zuri au anapenda kusema uongo! Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema mshwasha wa mawazo ya ubinafsi na kupata manufaa fulani ndiyo yanayomsukuma mtu kusema uongo. Ingawaje tabia njema zinataka kwamba hata kama maisha ya mtu yako hatarini, au mali yake au heshima yake bado mtu abaki kuwa mkweli. Tofauti kati ya mtu mkweli na asiye mkweli hudhihirika wakati wa majaribu na mitihani ambapo mtu muaminifu hubaki kung'ang'ania ukweli hata kama maslahi yake binafsi yatakuwa hatarini.

Siku hizi watu wanaoomba hifadhi hapa (Uingereza) na nchi zingine za Ulaya wanajiingiza kwenye uongo wakati wanapoomba msaada wa kisheria kwa mawakili, hii ni pamoja na hkhm kuendelea kuwaasa juu ya hili. Wanaeleza visa (hadithi) za kubuni ingawaje pamoja na hayo maombi yao yanakataliwa. Hapa na sehemu zingine za dunia kundi maalaum la mawakili limetengenezwa ili kuwasaida wale wanaoomba hifadhi, ambapo wanasheria huwasaidia kwa kuwapatia muongozo ufaao.

Rais wa mawakili hawa mara kadhaa hunieleza kwamba kesi hii na ile imetupiliwa mbali kwa sababu kulikuwa na maelezo mengi ya uongo ndani yake. Uwongo husemwa kwa maslahi ya kidunia bila kufikiria kwamba Mwenyezi Mungu ameutaja uongo na shirki kwa kuviambatanisha (kuwa kitu kimoja). Kisha kuna wengine hutumia uongo ili kupata maslahi yatolewayo na serikali. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema kwamba uongo ni sawa na sanamu na yeyote anayeutegemea anapoteza matumaini ya kumtegemea allah.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. pia alichukua ahadi kwetu ya kwamba tutajiepusha na uzinzi. Alisema msiukaribie uzinifu. Hii inamaanisha kujiepusha na hata yale mazingira ambayo yanaweza kuamsha hisia tu za uzinzi na msikanyage njia zile ambazo zina hatari ya kuangukia kwenye kosa hili. Siku hizi filamu chafu kabisa zinaoneshwa kwenye televisheni na pia kwenye intaneti au zinaweza kupatikana kupitia humo. Hii ni zinaa ya macho na kifikira na ni chanzo cha kuangukia kwenye tabia zingine chafu.

Mambo haya pia yanapelekea pia kuziporomosha nyumba (familia). Akinamama huniandikia juu ya waume zao wanaoangalia picha chafu kupitia intaneti kutwa mzima na vivyo hivyo baadhi ya

akinababa huniandikia juu ya wake zao wanaofanya hivyo. Hatimae mambo huishia kwenye khulaa au talaka. Filamu hizi pia zinawapelekea watu wawe na tabia mbaya kuliko wanyama. Jamii ya Kiahmadiyya kwa ujumla wake inajitenga na tabia hizi chafu hata hivyo iwapo juhudi kubwa na ya kukusudia haikufanyika ili mtu kujilinda mwenyewe akiwa anaishi kwenye mazingira haya hakuna uhakika wa kupata utakaso. Kuna haja ya jambo hili kuzingatiwa sana.

Ahadi nyingine tuliyochukua kwa Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) ni kujitenga mbali na makosa ya jicho. Qur'ani imetoa amri ya (ghadhul Basar) kuzuia jicho na Mtume (amani na baraka za Mwenyezi Mungu iwe juu yake) alisema kuwa moto umeharamishwa kwa lile jicho ambalo linajizuia kutokana na kuangalia kile Mungu alichokataza. Masihi Aliyeahidiwa (ambaye amani) akasema: Tumepewa fundisho jema la kuamrishwa kutokuangalia wanawake na uzuri wao ambao wako nje ya mipaka ya kisheria (ambao si ndugu wa karibu)

Alisema kutojizuia katika kuangalia wakati mwingine hupelekea maanguko. Mwenyezi Mungu ametupatia fundisho hili zuri kwa sababu anapenda kwamba macho yetu, nyoyo zetu na fikra zetu daima zibaki zikiwa safi. Islam imeweka mipaka hii kwa jinsia zote wanawake na wanaume. Wakati ambapo wanawake wameamriwa kujisitiri kuvaa hijabu (purdah) wanaume wameamrishwa kuzuia jicho. Kuna haja ya kutafakari ni kwa kiwango gani tunalitekeleza hili pia.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amechukua ahadi kwetu kwamba daima tutajitenga mbali na njia zote za uovu na ufisadi. Kwa hakika ni uovu kwenda nje ya amri za Mwenyezi Mungu. Mtume mtukufu s.a.w. wakati fulani aliwahi kuonesha kwamba kusema maneno ya matusi ni uovu na ufisadi.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliwahi kusema imethibitika kutoka ndani ya Quran tukufu kwamba mtu mfisadi na muovu ndiye atakayeadhibiwa mwanzoni kuliko mpagani. Zama ambapo waislamu walichupa mipaka ya uovu na ufisadi na kutokuheshimu amri za Mwenyezi Mungu na wakazama kwenye mapenzi ya dunia hapo Mwenyezi Mungu aliwaangamiza kupitia watu kama Halagu na Genghis Khan. Hali ya waislamu leo ni kama hiyo.

Ahadi nyingine ambayo tumefanya na Masihi Aliyeahidiwa a.s. ni hii kwamba tutajitenga na ukatili.

Ukatili kwa hakika ni kosa kubwa. Mtume mtukufu s.a.w. akielezea makosa miongoni mwa makosa makubwa alisema. Iwapo mtu atadhulumu hata upana wa kiganja kimoja tu cha ardhi kutoka kwa ndugu yake basi udongo wote ulio chini ya kipande hicho hata chembe ndogo kabisa hivyo vyote vitawekwa kama kola (mzigo mzito) shingoni mwake siku ya kiama. Kwa hakika ni jambo linalotakiwa kukumbukwa sana isije ikawa kwa sababu ya ubinafsi watu wanadhulumu haki za wengine mahakamani. Hili nalo ni jambo ambalo twapaswa kuliweka maanani sana.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. pia alichukua baiat kwetu kwamba tutajitenga na kukhini (khiyanat) yaani kutokuwa mwaminifu / kuvunja amana. Kipimo cha kutekeleza amri hii kiliweka na Mtume mtukufu s.a.w. aliposema: Usifanye hiana hata kwa mtu ambaye yeye amekufanyia hiana. Hivyo hakuna kisingizio chochote kinachokuruhusu kufanya hiana. Iwapo Ahmadiyya Fulani atakudhulumu omba ushauri kutoka Bodi ya Qadha na iwapo yeyote nje ya Jumuiya amekudhulumu pata omba ushauri ndani ya Jumuia au Jumuiya itakushauri kuchukua hatua za kisheria.

Ahadi nyingine ambayo imechukuliwa kwetu na Masihi Aliyeahidiwa a.s. ni hii kwamba daima tutajitenga na fujo na kuvunja sharia. Wakati ambapo halitakiwi lizuke swala la kufanyiana fujo na utovu wa nidhamu miongoni mwetu, mafundisho ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. yanatutaka kwamba tusiwafanyia fujo wala kuwatendea kinyume na nidhamu hata wale wanaotukandamiza. Alisema: Msipambane kwa uovu na wale wanaokupingeni (wanaokukimbieni na kukunyapaeni) kwa sababu tu mmejiunga na Jumuiya hii iliyoanzishwa na Mwenyezi Mungu, badala yake waombeeni wakati mkiwa faragha.

Sikilizeni! Nimeamriwa mara kwa mara nikufahamisheni kwamba daima jiepusheni na mahala pale palipo na fujo na uvunjifu wa nidhamu. Kuweni wavumilivu wakati mnapotukanwa na jibuni uovu mnaofanyiwa kwa wema. Ni jambo jema kwenu iwapo mtaondoka mahala pale ambapo kuna mtu anayeelekea kusababisha fujo na kuvunja nidhamu na mumjibu au mkabiliane naye kwa upole. Ni jambo nisilolipenda kabisa ninaposikia kwamba mtu fulani wa Jumuiya yetu amemfanyia fujo au kumvunjia heshima mtu fulani. Mwenyezi Mungu naye hapendi kabisa kwamba Jumuiya hii ambayo

ameikusudia kuwa ya mfano wa kuigwa mbele ya dunia ishike njia zisizo za kitawa.

cIwapo nasaha hizi za Masihi Aliyeahidiwa a.s. zingeshikwa kuhusiana na kuwatendea wake, ndugu na wengine pia tusingekuwa na hata hii mifano kidogo (ya vurugu) ambayo tunaiona ndani yetu au angalau ingepungua sana.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. pia alichukua ahadi ya kiapo kwetu kwamba daima tutajiepusha na uhaini. Iwe ni kwa mtumishi wa kawaida wa Jumuiya au kwa serikali iliyopo madarakani. Zaidi ya jambo ambalo serikali inajaribu kuingilia masuala ya kiimani ya mtu fulani, sio fundisho la kiislamu kabisa kuwa na hata wazo la kihaini kwa serikali na mtu kuchukua sharia mikononi mwake au kuwashawishi wengine kufanya hivyo.

Pia tumetakiwa tusijiwachie kutekwa na tama za nafsi. Kuna njia nyingi za mtu kutekwa na tamaa za nafsi yake kupitia televisheni na intaneti, zaidi ya hayo magomvi mengi na mikwaruzano inaanzia hapo. Ni jukumu la kila Ahmadiyya kuhakikisha kwamba najitenga mbali na hata jambo dogo kabisa linaloamsha hisia za kinyama au linalopelekea mtu kujisahau.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema baada ya kujiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya

***Endelea uk. 4***

# Khalifa mtukufu aombea kheri ya mwaka 2015:

*Kutoka uk. 3*

mtu ashike kiapo kwamba atatekeelza sala zote tano kwa nyakati zake na masharti yake yote. Sala ni faradhi ya lazima kwa kila mtu na hata mtoto aliyefikia umri wa miaka 10 na wazazi wanatakiwa waliangalie hilo kwa umakini. Jambo hili linaweza tu kutimiziwa haki zake iwapo wazazi pia watasimamisha sala zao kwa umakini. Malalamiko mengi yanapokelewa kuhusu jambo hili; baadhi ya watoto husema kwamba wazazi wao hawasali ipsavyo na wake pia husema waume zao hawatekelezi sala ipasavyo.

Kwa mwanamume kutekeleza sala kwa kujali sharti zake zote ni pamoja na kusali jmaa miskitini mara tano kwa siku isipokuwa kama kuna sababu ya kimsingi kama vile ugonjwa. Kama hili lizingatiwe misikiti yetu ingejaa. Iwapo hata viongozi wa kiofisi tu wangelilizingatia hili hali ingebadilika sana. Juhudi maalum inahitajika juu ya hili na viongozi wa Jamaat pamoja na wale wa Tanzeem wanatakiwa kulizingatia hili. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema ikiwa mtu anawaza kuiacha sala basi aelewe kwamba hawezi kufikia popote zaidi ya pale walipo wanyama.

Ahadi pia inachukuliwa kwamba tutajipanga kusali sala ya Tahajjud. Tahajjud ni lazima isaliwe kwa sababu hiyo ndio njia waliyopita wachamungu waliotutangulia na ndio njia ya kujipatia ukaribu na Mwenyezi Mungu. Pia kusali tahajjud kunamkinga mtu na makosa na tabia mbaya na pia kumkinga na magonjwa mengi ya kimwili. Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema Wanajumuiya wa Jumuiya yetu ni lazima isali Tahajjud kwa kudumu. Ikiwa hawawezi kusali rakaa zote basi angalau wasali hata rakaa mbili. Umakini unatakiwa kuwekwa juu ya hili.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amechukua ahdi kwetu ya kudumu (kufanya duruud) kumsalia Mtume s.a.w. Mtume mtukufu s.a.w. amsema: Mwenyezi Mungu atamrehemu mara kumi zaidi Yule mtu ambaye ananisalia na kunitakia rehema mimi. Hazrat Umar r.a. alisema: Dua yoyote ambayo inaombwa inabakishwa baina ya mbingu na ardhi na haipandishwi juu (kukubaliwa) hadi pale muombaji atakapomsalie Mtume mtukufu s.a.w..

Ahadi nyingine tunayoichukua ni ya kudumu kuomba Istighfar (kuomba msamaha wa makosa na mapungufu yetu). Mtume mtukufu s.a.w. alisema: Mwenyezi Mungu humfungulia njia za kumuepusha na majanga na kumsogeza kwenye ufaulu mtu yule anayefanya isitighfar kwa wingi sana na pia humruzuku kwa namna asiyoitarajia. Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema: Baadhi ya watu wanajua jambo Fulani ni kosa wakati baadhi yaw engine hawajui. Hii ndio sababu Mwenyezi Mungu ameagiza kufanya isitighfar kwa kudumu. Hivyo mtu Yule anayeleta Isitighfar anaomba msamaha kwa makosa yale anayoytajua na asiyoyajua na makosa yale yaliyo dhhairi na yaliyofichikana kwake. Hivyo umuhimu wa kuleta isitighfar daima uwe mbele ya macho yetu.

Ahadi nyingine ni hii kwamba daima tutazikumguka hisani za Mwenyezi Mungu zilizo juu yetu. Na hisani kubwa kabisa ya Mwenyezi Mungu ni hii ya kutuwezesha kumtambua imam wa zama. Iwapo tutaizingatia neema hii tutavutwa kwenye kuwa na mafungamano yaliyohalisika na Masihi Aliyeahidiwa a.s. na tutapata nguvu ya kutekeleza mafundisho yake kwa matendo.

Pia tunachukua ahadi ya kumtukuza na kumsifu Mwenyezi Mungu. Mtume mtukufu s.a.w. alisema kazi yoyote muhimu ambayo hainzi kwa kutaja sifa za Mwenyezi Mungu jambo hilo linakosa Baraka na athari njema. Na mtu

ambaye hana shukurani kwa kidogo pia hawezi kushukuru kwa kikubwa na mtu yule ambaye hawashukuru watu pia hawezi kumshukuru Mwenyezi Mungu. Hivyo tumtukuze Mwenyezi Mungu kwa namna ambayo pia tutatoa shukurani kwa viumbe wake.

Pia tunachukua ahadi kwamba hatutosababisha maumivu yoyote kwa kiumbe chochote cha Mwenyezi Mungu. Pia tunachukua ahadi hasa ya kutkumletea dhara mwislamu yeyote kutokana na matamanio yetu maovu na kwmaba tutawasamehe watu kwa kadri iwezekanavyo. Ingawaje iwapo hakuna njia nyingine na watu wengine wanapita mipaka ya uonevu tutijulisha mamlaka. Jambo hili nalo tutalifanya kama njia ya kuleta usuluhishi au matengenezo na sio kwa sababu ya uadui binafsi au hamaki. Jambo la matengenezo (kutoa adhabu) litafanywa na wale waliopo madarakani ambapo nao wanatakiwa wafanye bila ya ubinafsi au faida Fulani. Kwa ujumla muda wote mtu abaki kuwa mpole na mnyenyekevu.

Pia tumechukua hadi kwamba muda wote tutabaki kuwa waaminifu kwa Mwenyezi Mungu katika hali zote. Mtume mtukufu s.a.w. alisema: Mambo ya mwaminio ni ya ajabu sana. Kila jambo alifanyalo linakuwa na Baraka. Na Baraka hii ni maalum kwa ajili ya mwaminio tu. Wakati anapopata neema yoyote, au furaha humshukuru Mwenyezi Mungu na jambo hile hupelekea kubarikiwa zaidi. Na pia anapopata shida yoyote au mateso au hasara, hufanya subira na jambo hilo pia huwa ni sababu ya kupata Baraka na malipo mema kwa subira yake.

Kwa hakika mwaminio wa kweli humkimbilia Mwenyezi Mungu katika hali zote na kwa njia hiyo ndipo kiapo cha kuwa radhi na mipango ya Mwenyezi Mungu na kukubali shida na maummivu katika njia ya Mwenyezi Mungu kinaweza kutimizwa. Masihi Aliyeahidiwa a.s. masema; wale walio wa kwangu hawawezi kutenganishwa name, sio kwa sababu ya mateso ya watu wala kwa mitihani na majaribu kutoka mbinguni. Tutabaki kuwa pamoja na Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na tutaendelea kutokujali kudhalilishwa au maumivu katika njia hii. Hiki ni kiapo chetu.

Pia tunachukua ahdi wakati wa baiat kwamba hatutofuata mila zisizo za kiislam. Mtume mtukufu s.a.w. alisema: mtu yoyote anayeanzishwa mila kwa jina la dini ambayo haina uhusiano wowote na dini, mila hiyo itamlaani na haitopokelewa. Ni lazima tuwe makini juu ya hili. Mila nyingi a kimakosa kwenye ndoa zimebuniwa ambazo inabidi ziepukwe na kila Ahmadiyya na pia tusijiwachie kuathiriwa nay ale yanayoendelea kwa wale waliotuzunguka. Huzur alisema ameshaliongelea jambo hili kwa kina siku zizlizopita. Makatibu wa Tarbiyyat na masadr wa Lajna Ilamillah wayaibue mambo haya kila wakati ili kwamba wanajumuiya waweze kukingwa dhidi ya makosa haya.

Ahadi nyingine ni kujizuia dhidi ya kuangukia matamanio ya kidunia. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema: Pepo ni daraja ambayo inafikiwa na mtu yule anayehofia kusimama mbele ya Mola wake na hivyo anajitahidi kujizuia kumezwa na tamaa zake mbaya. Mtu kujizuia asiangukie tamaa za kidunia ni kujitoa moja kwa moja kwa ajili ya Allah. Kwa njia hii mtu anapata radhi ya Mwenyezi Mungu na anaipata pepo kwenye dunia hii hii.

Ahadi nyingine ni kujisalimisha chini ya ufalme wa Quran tukufu. Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema; Shikeni hadhari na msiinue hata hatua yenu moja kinyume na fundisho la Mwenyezi Mungu na la Quran tukufu. Ninakuambieni kwa ukweli kabisa mtu yule ambaye anakiuka hata amri moja miongoni mwa amri mia saba za Quran tukufu anajifungia mlango wa wokovu kwa mikono yake mwenyewe.

Pia tunachukua ahadi kwamba tutalifanya kila neno la Qurani na kila kauli ya Mtukufu Mtume s.a.w. kuwa msingi wa mwongozo wetu. Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema: Tunaye Mtume mmoja tu (ambaye ni Mtume Mtukufu Muhmmad s.a.w.) na tunayo Quran moja iliyoshushwa kwa Mtume mtukufu s.a.w. na kwa kuifuata hiyo tunaweza kumuona Mungu.

Pia tunakula kiapo kwamba tutajiepusha kikamilifu na kiburi na majivuno. Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema: Ninasema kwa ukweli kabisa kwamba katika siku ya malipo baada ya ushirikina hakuna kosa litakalokuwa kubwa kushinda kiburi. Hilo ni kosa kubwa kiasi hiki kwamba linamdhalilisha mtu katika dunia zote mbili. Hili ni jambo kubwa linalotakiwa kuangaliwa kwa umakini. Pia alisema: Ninaisihi Jumuiya yangu kujiepusha na kiburi kwa sababu kiburi ni kosa linalochukiza sana mbele ya Mungu.

Ahadi nyingine tuliyochukua ni kujitahidi kushika unyenyekevu. Mtume mtukufu s.a.w. alisema: Mtu yeyote anayeshika unyenyekevu na upole kwa ajili ya Allah, Allah atamuinua hadi uwingu wa saba. (atampa daraja ya juu peponi).

Tumechukua ahadi pia ya kwamba daima tutabaki wenye furaha (kwa kuridhika juu ya mipango ya Mungu). Jambo hili pia lapaswa kuzingatiwa na kila mmoja

Pia tumechukua ahadi ya kupitisha maisha yetu kwa uvumilivu na upole. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema: Ikiwa unataka kumuona Mungu mtafute karibu na nyoyo za watu wapole.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amechukua ahadi kwetu kwamba daima tutaichukulia imani na njia ya Islam kuwa kitu kinachopendwa zaidi kwetu kuliko maisha yetu, mali zetu na heshima zetu.

Ahadi nyingine tuliyochukua kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. ni kuwahudumia viumbe wa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema: Kumbukeni Mwenyezi Mungu anapenda utawa (wema) na anapenda pia viumbe wake wajaliwe (watendewe kwa wema). Wale wote kati yenu ambao wameungana nami hawana budi wakumbuke kumjali kila mtu bila kuangalia ni dini gani anayoifuata na ni lazima watende wema kwa kila mtu bila ubaguzi wowote kwa sababu hivi ndivyo Qurani inavyofundisha.

Ahadi nyingine tuliyochukua kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. ni kuwanufaisha viumbe wa Mwenyezi Mungu kwa kadri ya zile neema na vipaji tulivopewa sisi na Mwenyezi Mungu. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema: mwanadamu anayo mahitaji mengi na kutokana na sababu kadhaa wengine ni tegemezi kwa wengine. Hivyo kwa moyo safi kabisa na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu mtu ajaribu kwa unyofu (ikhlaswi) kabisa, bila ya ubinafsi na kwa kuwahurumia awanufaishe wanadamu kwa kadri awezavyo. Mtu amsaidie kila mwenye haja kupitia zile neema alizoruzukiwa yeye na Mwenyezi Mungu na ajaribu kwa juhudi kubwa kuyafanya maisha yao ya hapa duniani na ya akhera kuwa maisha bora.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. pia amechukua kiapo kwetu kwamba kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu tutaingia kwenye mahusiano ya kidugu naye (Masihi Aliyeahidiwa) na katika ahadi hii ya udugu tutaonesha mafungamano ya utiifu na kujitolea kwake kwa namna ambayo haiwezi kuonekana kwenye mahusiano na mafungamano yoyote ya kidunia yanayohitaji kujitolea na kutumikia. Hii ina maana kwamba tutamtii yeye katika kila jambo (jema) ambalo ametuelekeza kwa ajili ya manufaa / maendeleo yetu wenyewe na daima tutayatii yale tutakayoelekezwa na makhalifa wake baada yake. Fundisho hili ni kwa ajili ya kuihuisha sheria na linatokana na mafundisho ya Quran na hadithi za Mtume mtukufu s.a.w. na (sunnah) mwenendo wake uliobarikiwa. Bila ya hivyo haiwezekani kamwe tupate maendeleo na haiwezekani kamwe tubaki kuwa wamoja.

Kuna haja kubwa basi ya kujitathmini sisi wenyewe ni kwa kiwango gani tumeweza kutimiza viapo vyetu hivyo katika mwaka uliopita na iwapo kulikuwa na mapungufu yoyote tuangalie ni vipi tutaweza kutenda vizuri zaidi katika mwaka huu. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema: Aliyejiunga na Jumuiya yetu ni yule mtu tu ambaye anayafanya mafundisho yetu kuwa ndiyo (modus operandi) njia / mfumo wa maisha yake na anajitahidi kuyaingiza katika matendo yake kwa kadri ya uwezo wake.

Mwenyezi Mungu atusamehe mapungufu yetu na madhaifu yetu ya mwaka uliopita na atuwezeshe katika mwaka huu kufanya juhudi mwisho wa jitihada zetu katika kuyafuma maisha yetu yaendane sawa na matarajio ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. Mwenyezi Mungu atusaidie sana.

***Endelea uk. 5***

# Mahafali ya Kihistoria – 2014

*Kutoka uk. 2*

shule yetu kwa sasa ni Tshs. 1,000,000/= Kwa wanafunzi wa bweni na Tshs. 500,000/= kwa wanafunzi wa kutwa. Vile vile yapo mahitaji mengine ambayo mwanafunzi huchangia kadri yatakapohitajika mfano, ada ya mitihani, vitabu, mchango wa taaluma, sare ya mwanafunzi, godoro n.k.

Baada ya hotuba ya meneja wa shule, ratiba ya ukumbini ilisitishwa kwa saa mbili. Sambamba na mapunziko hayo, tulisali sala ya Adhuhuri na Alasiri. Na baadae dhifa kubwa ya kufa mtu ilifanyika. Pilalu na wali wa maji ni vitu vya kawaida katika sherehe mbalimbali, lakini unapoongelea kuku,La haula!, ni hatari. Kuku walimwagika kiasi ambacho kila aliyehudhuria aliridhika. soda na maji achilia mbali matunda, tumbo lilikosa nafasi ya kuviweka. Tunamuomba Allah mahafali yajayo yawe yenye mafanikio zaidi na zaidi.

Saa tisa kamili watu walirudi katika ukumbi kumalizia hatua iliyobaki. Kikao hiki kiliendeshwa na mmiliki wa shule Amir Sahib, Sheikh Tahir Mahmod Choudhry ambae baada ya usomaji wa Quran Tukuf iliyosomwa na Mwalimu Hamidii Kaigwa sura **18:61-71**. Huyu ni Mkuu wa shule Msaidizi,na shairi lililosomwa na Jalalaluddin Malik Mbawala (mwanafunzi) Shairi lisemalo "**Uidumishe Jalali, Shule ya Ahmadiyya",** alimkaribisha Mwenyekiti wa wazazi Bw, Aziz Ahmad Ng'amilo aseme machache kwa niaba yao. Bw, Ng'amilo akiwashukuru walimu na uongozi wa shule alisema; bila shaka uongozi wa shule umekabiliana na changamoto nyingi, lakini mara zote changamoto hizo zilijadiliwa kwa hekima na upendo na kamwe hazikuchukuliwa kama jambo la kuwakatisha tamaa viongozi na wallimu, bali kuwapa mbinu zaidi za kuiendesha shule. Hivyo ninakuombeni walimu msirudi nyuma bali mzidishe kasi zaidi ya kuiendesha shule hii. Nasisi wazazi tupo nyuma yenu. tutajitahidi kutoa ushirikiano kwenu ili kuleta maendeleo mazuri katika shule yetu.

Lilikuwepo neno la shukurani kutoka kamati ya kwanza kabisa ya uendeshaji na ujenzi wa shule hii. Mwl Abdullah Khamisi Mbanga alikaribishwa na alianza kwa kusema; Tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutimiza ndoto ya muda mrefu ambayo imetimia leo hii. Walikuwepo wazee kama Salum Kungulilo, Iddi Ramadhani, Ally Salum Ndendekile, Musa kiwanga, Mzee Msabaha n.k ambao waliomba usiku na mchana ili jumuiya iwe na shule yake, lakini hawakubahatika kushuhudia tunu hii . leo sisi tumeshuhudia tunayohaki ya kumshukuru sana Alllah.



*Amir Sahib Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akitoa hotuba (ambayo ilikuwa inatafsiriwa moja kwa moja) kwenye mahafali ya kidato cha Nne 2014 kwenye Shule ya Sekondari ya Ahmadiyya*

Akielezea changamoto walizokumbana nazo alisema; Amir sahib aliyepita Mzee Ali Saidi Mose aliunda kamati na akatukabidhi jukumu. Kamati hii ilikuwa haina chochote zaidi ya kuoneshwa sehemu ya kujenga tu. Lakini tulipigana kufa na kupona . Tulimuendea kila aliyekuwa mkereketwa wa shule ili achangie. Hatimae tukajenga darasa moja ambalo ndilo tulianza nalo. Mwalimu pia aliwaomba wazazi wawalete watoto wao. Wazazi wasifikirie faida ya kupata elimu ya dunia tu, bali hapa watapata vingi. Nidhamu, malezi bora ,watoto watajuana na pia watakuwa ni wenye kufanya ibada,hiyo ni faida kubwa zaidi.

Mwalim Mbanga pia aliwaomba vijana wa kiAhmadiyya wake kwa waume ambao wanamaliza na wale waliomaliza vyuo vikuu na kidato cha sita waje kujitolea katika shule hii.Pia aliwaasa wale ambao wanaacha kujitolea kwa sababu ya mapato kidogo. waige mfano wa marehemu Sheikh Amri Abed Kaluta ambae aliacha kazi ya malipo ya Tshs 600 na akaamua kufanya kazi ya dini kwa malipo ya shilingi 30. Lakini mwisho wake Mwenyezi Mungu alimnyanyua hadi kuwa waziri katika nchi hii.

Baada ya hapo ilifikia utoaji wa vyeti kwa makundi tofauti tofauti kwa ajili ya kutambua mchango waliotoa katika shule. Hakika hapa palikuwa na tamasha la kufurahisha na kutia moyo sana. kulikuwa na vyeti aina ya ngao ambavyo ni vya kioo kitupu kinachoonesha hadi upande wa pili lakini katikati yake yamewekwa maandishi mazuri kutambulisha dhima aliyoichukua muhusika katika kuisaidia shule. Vyeti hivi vilienda kwa Amir Sahib, kamati ya kwanza ya shule na Tandhim za Majlis Khuddamul Ahmadiyya, Majlis Ansarullah na Majlis Lajna Imaillah. Vilikuwepo vyeti vilivyowekewa Frem ya kioo na vile vya lamination . Hivi vilikwenda katika makundi mbalimbali. Makundi hayo ni kundi la Wanajumuiya waliojitolea kwa hali na mali, walimu waliotumia muda wao kujitolea tangu shule imeanzishwa,Mzazi aliyekuwa anamaliza ada kwa wakati, Mzazi aliyetoa ushirikiano kuisaidia shule kwa kiwango kikubwa, Mkuu wa shule wa kwanza, Viongozi walioitumikia shule, Wanafunzi saba waliosajiliwa siku ya kwanza shule inaanza, wanafunzi waliokuwa wakifanya vizuri kwa kipindi chote cha miaka mine, wanafunzi walio onesha nidhamu ya hali ya juu, Maendeleo mazuri ya kidini na mwisho vilitolewa vyeti kwa wanafunzi wanaohitimu kidato cha nne kutoka wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi vinavyothibitisha kuhitimu kwao, yaani (Living certificate).

Hatimae Hotuba ya mwisho ilitolewa na Mwenye shule, Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya waislam waAhmadiyy-Tanzania. Katika hotuba yake, Amir Sahib alimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufanya Mahafali haya ya kihistoria. Pia alitoa shukurani kwa kamati ya shule iliyopita na iliyopo hivi sasa, walimu , wanafunzi na wanajumuiyya ambao wamekuwa ni washiriki kwa kiasi kikubwa katika shule yetu hadi kufikia hapa.

Amir sahib akijibu risala juu ya changamoto mbambali zilizowasilishwa mbele yake hususan ya mwalim wa taaluma na ile iliyotolewa na wanafunzi wanaohitimu ambayo iliwasilishwa na Abdul-aziz Aziz Ng'amilo aliahidi kuwa, kwa ajili ya maendeleo shule, jamaat itajitahjidi kuisaidia shule kila inapowezekana. Kwa mnasaba huo, hivi karibuni tunataraji kuweka solar panel (umeme wa miali ya jua) katika eneo letu. Hii itatusaidia kupata umeme pia kwa ajili ya pampu za kusukumia maji na hivyo kumaliza tatizo kubwa la maji na umeme.

Amir akiongelea juu ya mipango ijayo alisema; nimewahi kuwa mbashiri katika nchi ya Ghana na Uganda katika miaka ya themanini na tisini, wao wanazo shule nyingi, hapa pia ni shauku yangu tuwe na shule nyingi zaidi. Mwaka jana tumeanzisha Nursary schoo (chekechea) katika Mkoa wa Morogoro, na hivi karibuni Humanity first America inatarajia kujenga shule ya msingi huko huko Morogoro. Akiongelea juu ya malezi ya vijana, Amir Sahib aliwataka sadr wa khuddamul Ahmadiyya na Lajna Imaillah kuangalia maendeleo na elimu ya kidini ya vijana waliopo mashuleni. Najua shuleni kuna mitaala ya masomo ya dini kutoka wizarani, Lakini ni wajibu wenu nanyi kufanya jitihada kuwaelimisha vijana wenu misingi ya imani yetu. Wapo ambao wanakwenda shule za bweni, ni vema muandae kambi za tarbiyyat (malezi) katika vipindi vyao vya likizo. Mwaka jana katika kipindi cha likizo, Jamaat iliandaa Tarbiyyat camp katika Mikoa ya Morogoro na Songea. Mwaka huu tunataraji kuandaa katika Mikoa ya Morogoro, Songea na Mtwara. Hivyo zitumike nafasi hizo vizuri katika kuwajenga vijanawetu kiimani.

Juu ya wanafunzi wanaohitimu, Amir Sahib aliwatakata wayatekeleza kwa vitendo yale yote waliyoyapata hapa huko waendako.kwani kupata tu pongezi hakumfanyi mtu kuwa bora, bali kutekeleza kwa vitendo yale waliyo jifunza.

Mwisho alitoa shukurani kwa watu wote waliohudhuria katika hafla hiyo na akaongoza maombi ya kimya kwa ajili ya kuhitimisha mahafali hayo.

Hakika yalikuwa ni mahafali yenye shani ya aina yake. wakati wa hotuba mbalimbali zilizokuwa zikitolewa, kulikuwa kuna mashairi murua yaliyokuwa yakighaniwa na wanafunzi kuanzia wale wa kidato cha kwanza hadi cha nne.

Wanafunzi wa kidato cha kwanza wavulana walikuja na shairi la kuwaaga ndugu zao lisemalo **" Kwaheri ya kuonana"**, wakati wasichana wa kidato hicho, shairi lao lilisema **"Barakallahu lakum wabaraka 'Alaykum"**. Vijana wa kidato cha pili kibwagizo cha shairi lao kilisema**"Form four mwaondoka, Mwatuacha nahuzuni. Form four mwatutoka, Twawaaga kwaherini".** Kidato cha tatu walimtuma mghani wao Abubakar Mkoka akaghani shairi lenye kibwagizo **"Pengine Mwendako Mbali, Ila sio mwisho wa safari"**. Wahitimu nao hawakubaki nyuma. Pamoja na furaha ya kuhitimu, majonzi pia yaliwasonga. Wao walimtuma mghani mahiri bi Radhia Luhuna kughani shairi lisemalo "**Milima haikutani, Binadamu hukutana"**. Mwisho ni shairi la kikundi lililoongozwa na Mwalim Muhsin Abas Kaye lisemalo **"Kwaheri, kwaheri, kwaheri, kwaheri ya kuonana".** Masha Allah!, Hakika watu walitokwa na machozi.sijui yalikuwa ni ya furaha au huzuni!. Lakini kutokana na nyuso zao kuwa ni zenye bashasha, ni muhali mioyo kuwa kinyume chake. Alhamdulillah Rabbil 'Alamiin. Wazazi, walezi , ndugu na jamaa mbalimbali, walisheheni mataji ya maua, kadi na zawadi kedekede kwa ajili ya kutoa tunu kwa vijana wao. Fursa ilitolewa, na kila mmoja alikifu shauku yake katika kuwapongeza vijana wao sambamba na upigaji wa kumbukumbu za picha mgando.

Hakika mahafali hayo, yameacha athari katika mioyo ya wengi. kwetu ni siku ya kukumbukwa sana kwani tumeuangusha ukuta wa belin. Kizuizi kikubwa ambacho kiligeuka msamiati katika fikra zetu kuwa **hatuwezi.** Kwa msaada mkubwa wa Mwenyezi Mungu **Tumeweza**. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aiendeleze shule yetu na kuipa mafanikio makubwa tunayotarajia. Tunamuonba sana Mwenyezi Mungu afanye vijana wetu wapate matokeo mazuri ya mitihani waliyoifanya, Amin.

# Bustani ya Washairi

## *Majibu ya Utenzi wa Injili*

***Mtunzi:***
***Al-Ustadh Khamisi S.S. Wamwera***
***Kimbangulile - Mbagala Rangi Tatu***
***Dar es Salaam***

1 Kwa Jina lako Latifu
Mwenyezi Mkamilifu
Sisi kwako ni hafifu
Hakuna alozidia

2 Alozidia hakuna
Kukupita Maulana
Sote sisi ni watwana
Tuloijaza Dunia

3 Kusudi na nia yangu
Katika utunzi wangu
Ni kumjibu Mwenzangu
Kwa yale alotongoa

4 Mtunzi kajikalifu
Machache akaarifu
Ya Injili Takatifu
Ili tupate tambua

5 Katika kwake kunena
Mengi hayakulingana
Yesu kuwa Mungu Mwana
Ni moja alopotea

6 Sote tunavyofahamu
Toka enzi za Adamu
Mungu Mmoja dawamu
Hakipo cha kuzidia

7 Hata Nabi Selemani
Aliwafunza nsani
Mungu Mmoja Imani
Na wala hakupindua

8 Na Musa alipofika
Hakufunza kuwashika
Mola watatu shirika
Vipi Yesu kupotoka?

9 Sisi wote tunajua
Mungu Mmoja Rabua
Nani anayebeua
Kwa imani na sheria?

10 Anayebeua nani
Ni nani huyu ni nani
Atokeze uwanjani
Na sisi tunajitoa

11 Mungu Mmoja nasema
Hana Baba wala mama
Hana mwana si yatima
Wengine kusaidia

12 Hana mwisho hana mwanzo
Mmiliki wa mafunzo
Na ya kwamba ndiye chanzo
Haya yote twayajua

13 Tunajua bilkuli
Mungu Mmoja halali
Hasinzii wala hali
Ni sifa zake Jalia

14 Mfalme wa dunia
Nyota pamoja na jua
Mmoja hakupungua
Wengine kuzidishia

15 Hakupungua kabisa
Kabisa hana makosa
Utatu ni masakasa
Mbali twayatupilia

16 Kung'ang'ania utatu
Ni jambo la utukutu
Ndanimwe hamna kitu
Bali kani na udhia

17 Ati kuna Baba Mungu
Pia kuna Mwana Mungu
Kadhalika Roho Mungu
Kitu kimoja sawia!

18 Hawa waungu watatu
Wenye majina matatu
Iweje wewe si tatu
Mmoja akabakia!

19 Watatu wawe si tatu
Mmoja awe watatu
Si siri kufichwa watu
Na kuipotoa njia?

20 Lakini walo wajuzi
Wamekwisha kumaizi
Ya kwamba Mola Mwenyezi
Mmoja wa Azalia

21 Na mimi nina yakini
Kwako wewe naamini
Hautayatupa chini
Haya ninayokwambia

22 Huwezi kutumikia
Bwana watatu sikia
Bwana wa kweli Jalia
Nini kinawazuzua?

23 Kinawazuzua nini
Imani ya kipagani
Mnaitia kundini
Katika Umasihia?

24 Vipi mnadanganyika
Wapagani kuwateka
Dini yao mkashika!
Kisha mkafurahia?

25 Ola utatu wa Mungu
Ni fumbo gani wenzangu
Tangu kuumbwa kwa mbingu
Kwanza hivi twasikia

26 Ni fundisho la kinyume
Hawakufunza Mitume
Sisi vipi tuchutame
Hata kulifurahia?

27 Mwalifurahia vipi
Hali Mungu halimpi
Heshima japo ni fupi
Wenzenu tunashangaa

28 Ni heri kuliachia
Si mana kulishikia
Dhambi mnajichumia
Bileshi bila ya njia

29 Yesu takuwaje Mungu
Kaumbwa kaomba Mungu
Vipi tumpe kifungu
Kwamba Mungu mwana pia?

30 Ee, Bwana Mathiasi
Uandike kwa kiasi
Pamwe na hayo uhisi
Yepi yanaelekea

31 Usome na uchungue
Haya pia yakutue
Vyema nawe uyajue
Uloamba achilia

32 Achilia uloamba
Hayana ambayo kwamba
Ni fundisho la kufumba
Ni nani atafumbua?

33 Ni nani huyo ni nani
Atokeze kilingeni
Aseme hii imani
Ni wapi imetokea

34 Katika Amri kumi
Ndani yake hatusomi
Mungu watatu usemi
Vipi bwana kutwambia?

35 Yesu alikunywa maji
Kalala kala malaji
Msaada kashitaji
Vipi Mungu amekuwa?

36 Aliteswa huyu Yesu
Kwa jambo lisilohusu
Walakini majasusu
Ndio walipendelea

37 Hakika kitendo hiki
Yesu kutiwa mikiki
Dalili moja ya haki
Kwamba yeye si Jalia

38 Jalali hasulubiwi
Kuteswa kwake haiwi
Haonwi macho ya kiwi
Tangu kuumbwa dunia

39 Na Yesu wa Nazareti
Kawambwa katika mti
Ukazunguka umati
Wapate kumwangalia

40 Alipokuwa yu hoi
Kaomba hawamtoi
"Eloi Ewe Eloi"
"Mbona unaniachia?"

41 Kwa nini waniachia
Wayahudi waniua
Hali sinayo hatia
Kosa sikuwatendea

42 Mola ninayo yakini
Kwako Wewe naamini
Hautayatupa chini
Haya ninayokwambia

43 Aliyeitwa ni nani
Kama si Mola Manani
Na hii ndiyo yakini
Hakuna wa kukataa

44 Iwapo Yesu ni Mola
Binafusi hana hila
Mbona kamba "ala ala"
Kikombe niondolea?

45 Ola Baibo yasema
Tena bila ya heshima
Anayesemwa Karima
Yesu mwana wa Maria

46 Kwamba katengeza pombe
Kwenye arusi walumbe
Walipokunywa viumbe
Utamu kufurahia

47 Kiumbe huyu kiumbe
Mungu hatengezi pombe
Ninakana hata chembe
Hali hii kuingia

48 Iweje Yesu ni Rabi
Twajua yake nasabi
Imani yenu kharabi
Kharabi kitu kibaya

49 Sifa zake nyingi sana
Sifa zake Maulana
Za urefu na mapana
Siwezi kukadiria

50 Sifa zake Subhana
Zote siwezi kunena
Hana baba hana mwana
Pweke anaendelea

51 Mwenyezi Mungu Mjuzi
Yote hayamshangazi
Yesu hana sifa hizi
Vipi Mungu amekuwa?

52 Mungu Ajua Kiyama
Siku tutayosimama
Mbele yake kwa heshima
Hukumu kutupatia

53 Bali Yesu katamka
Ya kwamba hana hakika
Siku tutayofufuka
Lini itatufikia

54 Kadhalika akanena
"Anayejua hakuna
Roho hata huyo mwana
Bali mmoja sikia"

55 Mmoja huyo ni Mungu
Aliyetandika mbingu
Ameumba ulimwengu
Ndanimwe twaogelea

56 Mwenyezi Mungu ni mwema
Kwa kila hali nasema
Lakini Yesu si mwema
Mwenyewe anatwambia

57 Mtu mmoja maana
Alifika kuonana
Na Yesu kuulizana
Mambo yalimtatia

58 Kasema, "Mwalimu mwema
Ninautaka uzima
Nifanye nini mapema
Nataka kujiokoa"

59 Yesu katazama mbingu
Kasema kwa walimwengu

"Mwema Mmoja ni Mungu"
Hebu Luka chungulia

60 Baada kuona tata
Wakristo waleta
Hoja zisizo takata
Imani kujikuzia

61 Ati Yesu katengeza
Mingi sana miujiza
Dalili za kushangaza
Kwamba yeye Mungu pia!

62 Kwamba Yesu kafufua
Watu wengi kafukua
Ishara moja ya kua
Ya yeye kuwa Jalia

63 Hebu sasa tuchunguze
Kwa ndani tupeleleze
Nalo hili tumalize
Kwamba halina satua

64 Hizo zote si dalili
Za Yesu awe Jalali
Biblia yakubali
Mitume walipitia

65 Nianze kwa Ezekeli
Aliyekuwa Rasuli
Miujiza mingi kweli
Mingi aliyoitoa

66 Jeshi alilifufua
Mafupa lililokuwa
Wote aliwafufua
Hakuna alobakia

67 Alobakia hakuna
Wakubwa hadi vijana
Kawafufua mchana
Inasema Biblia

***Utaendelea toleo lijalo, Inshallah***

بسم الله الرحمن الرحيم

# JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA TANZANIA

## KALENDA YA MATUKIO KWA KIPINDI CHA JANUARI - JUNI 2015

| MWEZI | MWAKA | TAREHE | TUKIO |
|---|---|---|---|
| **JANUARI** | **2015** | 13 – 26 | Ahadi mpya` za Waqf-e-Jadid kwa mwaka 2015. |
| | | 24 – 31 | Wiki maalum ya makusanyo ya mchango wa kawaida. |
| **FEBRUARI** | **2015** | 02 – 08 | Siku maalum za kuwaalika wageni kwa mazungumzo katika Jamaat zote. Taarifa zitumwe Makao Makuu. |
| | | 20 | **Siku ya Mwana Aliyeahidiwa.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii). |
| | | 21 – 22 | Siku maalum za kuwatembelea wagonjwa, mahospitalini na majumbani. Pia kuwatembelea mayatima, walemavu, na vikongwe (washiriki, Ansar, Khuddam na Lajna). |
| **MACHI** | **2015** | 01 – 10 | Siku maalum za kufanya vikao vya kujadiliana ajenda za Shura ya mwaka 2015 na kuchagua wajumbe. |
| | | 15 | **Siku ya Seeratu Nabii.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii). |
| | | 14 – 15 | Mahubiri Maalum kwa kila tawi. (Viongozi wote ni lazima washiriki). |
| | | 20 | Mahubiri ya tarehe 14 – 15 yatolewe maelezo yake mbele ya Wanajumuiya wote. |
| | | 23 | **Siku ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii). |
| | | 31 | Siku ya mwisho ya kutuma dondoo za Mushawara kutoka matawini kwa ajili ya Shura ya mwaka 2015. |
| **APRILI** | **2015** | 05 | Mitihani kutoka kitabu cha: **Safina ya Nuhu.** |
| | | 05 – 12 | Siku maalum za kukusanya malimbikizo ya mchango wa Tahrik Jadid na Waqfe Jadid. |
| | | 25 – 26 | **Shura ya Kitaifa Dar es Salaam – mwaka 2015.** |
| **MEI** | **2015** | 08 –15 | Siku maalum za kukusanya malimbikizo ya michango. (Hasa mchango wa kawaida). |
| | | 15 | Wajumbe wa Shura wayaeleze matawi yao maazimio ya Shura - 2015 |
| | | 27 | **Siku ya Ukhalifa.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii hii). |
| **JUNI** | **2015** | 01 – 15 | Siku maalum za kuhakikisha kwamba kila Mwanajumuiya amekamilisha Bajeti ya michango yake hasa wa kawaida/Wasia sawa na kiwango cha kila mwezi. Juhudi maalum zifanywe. |
| | | 12 – 14 | **Ijtimaa ya Khuddamul Ahmadiyya Kitaifa.** |
| | | | **Ijtimaa na Shura ya Lajna Imaillah Kitaifa.** |
| | | 18 | ***Kuanza kwa mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani** |

*Zingatia: Saumu ya Ramadhani, itategemea kuandama kwa mwezi.

# Nafasi ya Qur'ani tukufu katika maisha ya kila siku ya mwaminio.

***Hotuba iliyotolewa kwenye Jalsa Salana 2014 na Mwl. Shamuni Juma***



***Mwl. Shamuni Mwishehe Juma akiwasilisha hotuba yake wakati wa Jalsa Salana ya 45 iliyofanyika Kitonga Dar es Salaam***

Nanyi humo mtapata vile zinazovipenda nafsi zenu nanyi humo mtapata vile mnavyoniomba" aya

Kufuata kikamilifu mafundisho ya Qurani tukufu ndio msingi mkubwa wa mafanikio ya Mtume (s.a.w). Na kama ilivyoelezwa na Hadhrat bi Aisha r.a kwamba Khulka ya Mtume s.a.w ni Qurani tukufu.

Ndugu zangu wapenzi katika maisha haya ya dunia yaliyojaa kila aina ya mabalaa, magonjwa, machafuko ya aina mbalimbali, mikasa, majanga na hatari nyingi za aina aina. Hakuna kilichobora kuliko kupata radhi ya yale ya aliyetuumba na akatujaalia macho, masikio, viungo, vitimilifu, akili, busara na hekima bure bila gharama yoyote. Katika aya hiyo Mwenyezi Mungu anatuahidi kuwa, kama tutadumu kumtumikia na kutangaza jina lake basi atawatuma malaika wake kuja katoa ulinzi maalumu kwa ajili yetu. Na haya ndio maelezo ya Masihi aliyeahidiwa pale aliposema:-

"Dunia ni mahali pa maelfu na malfu ya mabalaa, pia tauni ni moja katika hayo. Basi mshikeni Mwenyezi Mungu sawa sawa ili yeye ayatenge mbali mabalaa haya. "(SAFINA YA NUHU UK.9)

Taarikh ya islam na jamaat inathibitisha jambo hili, kwa kushika mafundisho ya Qurani tukufu iliyochanzo na chachu ya elimu na maarifa yote, Wengi wameinuliwa na kufika daraja za juu kabisa kiroho. Mawalii na wachamungu mbalimbali mameendelea kupatikana tngu zama za mtume mtukufu (s.a.w) na dunia imefaidika sana kwa sababu yao.

Waislamu walipolegea na kuiacha Qurani tukufu athari kubwa sana na mbaya zilitokea. Kwa fadhila za Allah akamtuma Masih aliyeahidiwa (a.s) ili kuja kufundisha na kuamsha ari ya kuipenda, kusoma na kuifuata Qurani tukufu. Matokeo yake ni kwamba waislamu wakaanza kupata tena mwamko na uhai wa kiroho. Mawalii na wachamungu wengine wamepatikana na wanaendelea kutoka katika jamaat ya Masih aliyeahidiwa (a.s)

Mtu kama vile Hadhrat maulana Nuruddin (r.a) ambae maisha yake yote yalikuwa ni mfano halisi kwa kila mmoja wetu na hili wala halihitaji maelezo marefu.

Mtu mwingine ni Hadhrat maulana GHULAM RASOOR (r.a) aliyezaliwa kati ya mwaka 1877 au 1879. Huyu alikuwa ni mchamungu wa hali ya juu kabisa na na alikuwa miongoni mwa masahaba wa Masih mau'uud a.s ambao wenywew ni dalili ya kweli wake. Maombi ya sahaba huyu (r.a) yalijaa shani ya ajabu na yalikubaliwa haraka sana na Mwenyezi Mungu. Katika moja ya matukio yanayokumbukwa ni pale alipoombwa na baba wa Dr Abdussalam ili amwombee mwanaye ambaye katika utoto wake (Dr Abdussalaam) alikuwa na matatizo ya kuzungumza. Baada ya maombi ya dakika chache, Hadhrat Maulana Ghulam Rasuu Rajeki alimwambia baba wa mtoto yakuwa:- "Wala msiwe na wasiwasi na mtoto huyu, wakati utafika yeye atazungumza na dunia yote itasikia"

Bishara hii ilitimia barabara, kwani mnamo mwaka 1962 alitoa hotuba kwa njia ya redio jijini London na mada yake ikawa ni "Atomiki kwa ajili ya amani" hotuba ambayo ilisikika duniani kote. Mtu ambaye hakuweza kuzungumza utotoni hatimayealikuja kujinyakulia tuzo ya Nobel katika sayansi akiwa ni mwislamu wa kwanza kupewa tuzo hiyo. Kutokana na matukio mengi ya aina hiyo akapatiwa lakabu ya kuwa yeye ni simu ya Mwenyezi Mungu.

Hapa Tanzania watu kama vile marehemu Sheikh Kaluta Amri Abeid, Marehemu mzee Rashidi Msabaha na wengine.

Mwingine ni Hadhrat Sir Zafrullah Khan r.a ambaye aliifanya Qurani tukufu kuwa tochi yake ya kila siku. Inasemekana kuwa siku moja alifuwa na wanafunzi kadhaa wa kiahmadiyya wakimuomba aweke saini - kama wafanyavyo watu mashuhuri hasa wanamichezo. Yeye aliwaambia kuwa watumie muda huo kwa kusoma Qurani tukufu, Hadithi za mtukufu mtume s.a.w, vitabu vya Masih aliyeahidiwa a.s na vya makhalifa waila yeye si chochote mbele ya vitu hivyo.

Yeye alikuwa mwislamu wa kwanza kusoma aya za Qurani tukufu katika vikao vya kinataifa.

Pia inaelezwa kuwa siku moja mchamungu huyu akiwa katika Kasri la Malkia wa Uingereza, huku mazungumzo yakiendelea baina yake na Malkia, muda wa sala ulifika akaangali saa yake na kuonyesha hali fulani ya mahangaiko. Malkia akamuuliza, je? Una ahadi na mtu yeyote? Akajibu ndio nina ahadi ha Mwenyezi Mungu, Muda wa sala umefika .

Hapo mazungumzo yakaahirishwa na akaandaliwa sehemu maalum kwa ajili ya kusali.

Hapa Tanzania wapo watu ambao wameingiza Qurani tukufu katika maisha yao ya kila siku na athari njema zimepatikana sio kwao tu bali hata kwa Jamaat na Taifa kwa ujumla. Watu kama vile marehemu Sheikh Karuta Amri Abeid, Marehemu Mzee Rashidi msabaha, marehemu Mzee Athumani Ndembo na wengi wengineo.

KURANI TUKUFU INAWEZA KUWAUNGANISHA WANADAMU

Qurani tukufu inasema: - 'Na shikeni kamba ya Mwenyezi Mungu nyote, wala msiachane' …(3:104) Faida nyingine ipatikanayo kwa kuifuata Qurani tukufu ni kuwaunganisha wanadamu na kuwafanya kitu kimoja kama inavyoelezwa katika aya hiyo hapo juu. Tukitwalii historia ya Islam tutagundua uwazi wa jambo hili. Waarabu waliokuwa wamegawanyika katika koo mbalimbali zilizozokuwa zinahasimiana kugombana na kupigana vita mara kwa mara zilisuluhishwa na mafundisho mazuri ya Qurani. Badala ya kuwa maadui , wakawa ni ndugu waliopendana kwa mapenzi ya hali ya juu kiasi kwamaba mfano wake haupatikani katika dunia. Qurani tukufu ikithibitisha hili inasema :- "Na ameunga mioyo yao, hata kama ungalitoa yote yaliyomo ardhini, usingaliweza kuiunga mioyo yao, lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyewaunganisha. Hakika mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, mwenye hekima". 8:64

Katika historia ya jumuiya hali hii inadhihirika wazi zaidi, na mkusanyiko huu wa Jalsa salana ni ushahidi tosha. Tumekusanyika hapa kutoka vijiji, kata. Tarafa, wilaya, na mikoa mbali mbali tukiwa na rangi na makabila tofauti tofauti, Lakini sote tunazungumza lugha moja tukichagizwa na kauli mbiu yetu ya, "Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote" Tukionganishwa na Masih aliyeahidiwa a.s ambaye ametueleza kuwa udugu huu ni bora kuliko wa Adamu, na ni bora kuliko uhusiano wa bwana na mtumishi wake.

Faida nyingine tunayoweza kuipata kwa kuishi sawa na mafundisho ya Qurani tukufu ni hii tunayofundishwa katika aya hii zifuatavyo:-

"Na anayemuomba Mwenyezi Mungu (Mwenyezi Mungu) humtengenezea njia ya kuokoka. Na humpa riziki kwa mahali asipopatazamia; na anayemtegemea Mwenyezi Mungu, basi yeye humtosha, kwa yakini Mwenyezi Mungu hutimiza kusudi lake. Hakika Mwenyezi Mungu amekwisha kiwekea kila kitu kipimo" .(65:3-4)

Historia ya islamu ni shahidi juu ya yote yaliyosemwa katika aya hizo. Mtume mtukufu (s.a.w) na hasibu yake mpenzi Hadhrat Abubakar Siddiq (r.a) waliokolewa katika pango la Thaur kwa sababu hii. Je?, Si kweli kuwa wale watatu walifunikwa na jiwe kubwa pangoni waliokolewa kwa matendo yao mazuri na kumuogopa kwao Mwenyezi Mungu? Bali hata katika nchi hii baadhi ya wanajumuiya katika sehemu mbali mbali wamepata kunusuriwa kwa namna za ajabu katika matukio tofauti tofauti ikiwemo hatari za samba nk. Pia aya inasema " Na humpa riziki kwa mahali asipopatazamia" Jambo hili linathibitika wazi katika historia nzima ya maisha ya Mtume Mtukufu s.a w ambapo baadhi ya wakati kulikuwa na shida kubwa ya chakula, maji n.k lakini kwa namna ya ajabu wakaondolewa kutoka katika shida hiyo.

Katika taarikh ya jamaat pia hali ni hiyo hiyo. Katika maisha ya Masih aliyeahidiwa (a.s) matukio kama hayo yametokea mara nyingi. Bali hata kwa masahaba wake (r.a) matukio kama hayo yameripotiwa kutokea mara kadha.

Inasemekana kuwa Hadhrat maulana Hakeem Nuruddin (r.a) mwaka fulani alikuwa bado hajamiliza ahadi yake ya mchango wa Tahriki Jadid na muda ulikaribia mno kuisha, Zikiwa zimebaki siku mbili au moja huku akiwa haonyeshi mahangaiko yoyote ghafla mtu mmoja alimjia baada ya sala ya alfajiri na kumkabidhi bahasha iliyokuwa na rupia mia moja ndani yake na akamwambia kuwa hiyo ni zawadi amemletea kutokana na huduma yake nzuri ya matibabu aliyompatia mama yake miaka kadhaa iliyopita. Pesa hiyo ilitosha kumaliza ahadi yake ya Tahriki jaded na kiasi kingine kubaki, Matukio ya aina hii yalikuwa mengi katika maisha ya Hadhrat Maulana Hakeem r.a

Tukio lingine linamhusu

***Endelea uk. 9***

# Muhammad Ibnu Siiriin: Mfalme wa taabiri za Njozi

**Mwl Abdullah H.Mbanga.**
**Ikwiriri- Rufiji.**

Miongoni mwa wataalam wa taabiri za njozi katika islam ni Imam Abu Bakr Muhammad bin Siiriin Al ansar Al Basrii (rh.a). Huyu ni mtawa aliyetunukiwa kipawa kikubwa cha uaguzi wa njozi. Imam Ibun Siiriin ndiye mwandishi wa kitabu maarufu cha taabiri za njozi kiitwacho AL MUNTAKHABIL KALAAM FII TAFSIRIL AHLAAM. Kitabu hiki kilipata umaarufu mkubwa katika ulimwengu kiasi hiki ya kwamba maulamaa wa baadaye wakakipa lakabu ya TA'BIIRU RU-YA KABIIR (yaani Tafsiri kuu ya njozi).

Imam ibun Siiriin Aliishi zama za Imama Malik bin Anas aliyekuwa kuwa mtaalam mkubwa wa Hadithi. Mji wa asili wa Ibun Siiriin uliitwa JIRJIRAYA, Huu ni mji mdogo uliokuwapo katika bonde lililo baina ya mito miwili mashuhuri, Euphrates (Furat) na Tigris kaskazini – mashariki mwa Baghadad. Baba yake, Siiriin alikuwa fundi maarufu wa masefuria ya shaba. Mama yake Safiyyah alikuwa na uhusiano wa karibu na Hadhrat Abu Bakr Siddiq. Ndoa ya mama huyu na Bw Siiriin ilisimamiwa na wake watatu wa Mtume s.a.w., pia ilihudhuriwa na masahaba wapatao 18 wa Mtume s.a.w miongoni mwa wale walioshiriki vita vya Badr. Kati yao alikuwemo Abi Ibun Ka'ab(r.a) ambaye aliongoza maombi katika ndoa hiyo. Mama huyu wa kihijaz alikuwa na taaluma ya kutia rangi katika nguo (batiki).

Muhammad bin Siiriin alizaliwa Basra mwaka wa 33 Hijria, yaani miaka miwili kabla ya kifo cha Hadhrat Uthma (r.a) khalifa wa tatu wa Mtume Mtukufu (s.a.w). Ibun Siiriin alikuwa na kipawa kikubwa cha uelewa tangu utotoni mwake. Alipenda mno kujifunza kurani, Hadithi na alikuwa na uchu mkubwa wa kutafuta elimu. Juu ya hayo alikuwa ni kijana mpole na mwenye hofu ya Mungu.

Hatimaye Ibun Siiriin akatokea kuwa miongoni mwa wapokezi wa hadithi wa kizazi cha pili, akiwa amepokea hadithi nyingi kutoka kwa masahaba wa mtume Mtukufu (s.a.w). Masahaba ambao Ibun Siiriin alipokea Hadithi kutoka kwao miongoni mwao ni Abu Hurayrah, Abdullah bin Umar, Zaid bin Thabit, Anas bin Malik, Abdullah bin Zubair, Ibun Hatim, Sulaiman bin Aamir, Ummu Atiyya Al-ansar (r.a) na wengineo wengi.

Katika harakati zake za kutafuta elimu, Ibun Siiriin alikuwa pamoja na watu ambao baadaye walijulikana kama matabii wa mwanzo ( yaani watu waliowaona na kujifunza kwa masahaba wa Mtume s.a.w). yeye alikuwa pamoja na abidah Sulaiman, Qais bin Abad, Salim bin Yasar, Rabii bin khaisham, Hamid bin Abdulr Rahman, Abdul Rahman bin Abu Bakr na dada wa Ibun Siiriin aitwaye Hafsah na wengine wengi.

Kutokana na bidii yake ya kutafuta elimu na kutokana na kipawa kikubwa cha uelewa allichojaaliwa, Ibun Siiriin akatokea kuwa kadhi wa kuaminika katika mji wa Basra, pia alikuwa mwalimu aliyebobea katika Tariikh (Historia), Akhlaq (utamaduni) na Fiq-h.

Ibun Siiriin pamoja na kuwa mwanachuoni aliyeaminika na kuheshimiwa sana, lakini hakuwa mtu aliyejibweteka. Alikuwa mchapakazi hodari aliyejihusisha na biashara katika mji wa Basra. Hali hii ilimfanya Ibun Siiriin awe mwanachuoni mwadilifu na asiyekubali kununuliwa kama ilivyokuwa kwa baadhi ya masheikh ambao walitegemea zaidi kufadhiliwa na jamii. Kutokana na hilo mara nyingi Ibun Siiriin alijikuta matatizoni baada ya kutofautiana na utawala katika baadhi ya fatwa zake. Mara kadhaa alionja ladha ya gereza na tabu mbalimbali za citisho kutoka serikalini. Hata hivyo Ibun Siiriin hakuwa mtu wa kupayuka kujibizana na kauli za watawala, bali yeye aghalabu alikuwa mtu mwenye kushikilia misimamo yake kwa upole lakini kwa imara zaidi.

La kupendeza zaidi ni kwamba alikuwa ni mtu mwenye kuheshimu sana mamlaka ya Dola . Hata alipoadhibiwa na Dola kwa uonevu bado alionyesha heshima na uaminifu mkubwa juu ya adhabu aliyopewa.

Inasimuliwa kwamba wakati Fulani Ibun Siiriin aliingizwa gerezani, Bwana Jela (mkuu wa gereza) aliathirika sana na uchamungu wake na akawa akimheshimu mno. Ndipo akamwendea Ibun Siiriin na kumwambia, "u bwana mheshimiwa, nakuruhusu wakati wa usiku nenda ukalale na familia yako nyumbani, ifikapo asubuhi ndipo uje hapa gerezani". Ibun Siiriin alikataa tunu hiyo akasema; "Hapana, Wallahi siwezi kukuunga mkono katika kufanya hiyana dhidi ya Sulatani". Ibun Siiriin alifanya hivyo kutokana na Taqwa yake iliyotokana na mafundisho ya Islam yaliyosisitiza kutii wenye mamlaka. Hivyo alipingana na khilafu yoyote dhidi ya utawala hata kama ilikuwa ikimpa nafuu. Daima alipingana na utawala pale tu ulipoonekana kuingilia katika upotoshaji wa mafundisho ya dini.

Kwa muhtasari, historia ya Ibun Siiriin inamuonesha kuwa ni mtu aliyekuwa mchamungu na aliye mfano wa kuigwa, alikuwa ni mtu aliyejitambua na mwenye ujuzi mkubwa wa masuala ya dini. Alichukia mno kujikweza na hakupenda kusifiwa. Alipenda usafi na unadhifu. Alijitenga mbali na mambo ya kipuuzi na yenye kutia shaka. Hakuwa mwenye choyo na husuda.

Ibun Siiriin hakuwa na tabia ya kupayukapayuka. Alizungumza pale tu ilipomlazimu kuzungumza, waila alikaa kimya na mwenye tafakuri ya kina kwa kila jambo. Anao usemi wake mashuhuri dhidi ya tabia ya kupayukapayuka, alisema; "Lau angejua msemaji kwamba asemayo huandikwa basi yangepungua maneno yake".

Mara nyingi alipenda kuirejea aya ya kurani Tukufu isemayo; ili Allah Awatakase walioamini na kuwafuta waliokufuru (3:142) kasha aliomba baada ya kusoma aya hiyo: Ee Allah tutakase, wala usitufanye kuwa tuliokufuru.

Mara nyingi alipoombwa ushauri na watu alisema Mche Allah na utafute riziki yako kwa njia ya halali, kwani ukitumia njia ya haramu hautapata vingi katika vile uivoruzukiwa.

Ibun Siiriin aliandika vitabu kadha, lakini kilicho maarufu na kikubwa miongoni mwao ni kile kiitwacho AL MUNTAKHABIL KALAAM FII TAFSIIRIL AHLAAM, au kama kijulikanavyo kwa wadau mbalimbali TA'BIIRU RUYA KABIIR. Katika kitabu hicho kinacho hesabiwa kuwa ndicho kitabu cha kwanza kabisa cha tafsiri za njozi katika historia ya Islam, Ibun Siirin ametumia elimu ya ndani ya kurani Tukufu katika kutoa taabiri za njozi.

Kitabu hiki kikawa ndio msahafu wa njozi duniani. Kilizalisha wataalamu wakubwa wa taabiri za njozi. Kwacho Ibun Siiriin akatambuliwa rasmi kuwa Imam wa Taabiri za njozi.

Kitabu hiki kilitafsiriwa kwa lugha nyingi za dunia kutokana na umuhimu wake. Baadhi ya watu waliendelea kukichapisha na kukisambaza katika vyuo vikuu mbalimbali katika ulimwengu wa kiislam.

Watu wengi walijifunza taaluma ya uaguzi wa njozi kupitia kitabu hiki cha Ibun Siiriin walifanikiwa kuwa waaguzi wakubwa wa njozi , kiasi cha hata wao wenyewe kumudu kuandika vitabu vyao. Miongoni mwa watu walioendeleza kazi na taaluma hii ya Ibun Siiriin ni mwanazuoni maarufu, mzaliwa wa Nablus huko palestina, Sheikh Abdul Ghani Nablus, mwandishi wa kitabu kingine maarufu katika taabiri za njozi kiitwacho TA'TIIRUL ANAAM FII TA'BIIRUL MANAAM. Hiki kinashika nafasi ya pili baada ya kile cha Ibun Siiriin kwa mujibu wa wadau wa elimu hii.

Ibun Siiriin aliishi umri mrefu, takriban miaka themanini, umri wake wote aliutumia katika kufanya kazi huku akitafuta elimu na kufundisha. Alifikia daraja ya juu sana ya taqwa na ufahamu. Hatimaye aliungana na Mola wake katika siku ya Ijumaa, tarehe 18, Shawwal mwaka wa 120 Hijriya.

Mji wa Basra ulioshuhudia kuzaliwa kwake, ndio huohuo ulioshuhudia pia kifo chake.

Allah amstareheshe peponi nasi atunufaishe kwa elimu yake. Amin.

# Nafasi ya Qur'ani tukufu

*Kutoka uk. 9*

Hadhrat Maulana Ghulam Rasuul Rajeki (r.a) , Sahaba huyu maarufu wa Masih aliyeahidiwa (a.s) ambae alipata kupewa lakabu ya kuwa "Simu ya Mwenyezi Mungu" anaelezea tukio moja la kuvutia sana, Anasema Siku moja akiwa na MIAN GHULAM HAIDER walikuwa safarini kurudi kijijini kwao, safari ilikua ndefu na jua likazama na usiku ukaingia.Wakapata hifadhi katika msikiti fulani ambao ulikua hautumiki .Mwenzie aliugua na homa ilizidi kupanda ,hawakuwa na chakula na hoteli zote zilikwisha fungwa.Usiku wa saa8 Hadhrat Maulana Ghulam Rasuul Rajeki alitoka nje kwa ajili ya kupenga kamasi. Ghafla alimwona mtu aliye shika chapati za moto na bakuli la nyama za mchuzi na HALWA Maulana Sahib alimuuliza,"unamtafuta nani na hiki chakula umemletea nani? Yule mtu akajibu hivi" hivi vyote nimeleta kwa ajili yako''Maulana Sahib akamuuliza tena "vyombo hivi niviache wapi? Yule mtu akajibu "viache ndani Maulvi Sahib (r.a) anasema kuwa, sote tulikula na tulishiba kabisa. Matukio haya na mengine mengi yanaonyesha faida ya kuifuata Qurani tukufu katika fundisho la kumtegemea Mwenyezimungu.Tena sehemu ya aya hiyo inasema,"Na anaye mtegemea Mwenyezi mungu, basi yeye humtoshea".

Hii inamaana kuwa kama mtu afuate sawasawa fundisho hilo,Mwenyezi Mungu atakuwa msaidizi wake mkuu na kumkidhi mahitaji yake na kumwondolea mbali matatizo yake. Hii ni kama vile Hadhrat masihi mau'uud (a.s) alipopata mahangaiko kufuatia kifo cha baba yake, na Mwenyezi Mungu akampatia ufunuo mtukufu uliosema:- "Je, Mwenyezimungu hamtoshei mtumishi wake?" (39:37)

Hali ya baadaye ya Hadhrat Ahmad (a.s) inathibitisha kutimia kikamilifu kwa maneno hayo. Naye mwenyewe amenukuliwa akisema:-

"Makombo ya watu yalikuwa ndio chakula changu, lakini sasa ninalisha wengine wengi kabisa." Bila shaka sisi sote ni mashahidi wa kutimia kwa maneno hayo. Kwa kifupi nikuwa kama mwanadamu aingize fundisho katika maisha yake ya kila siku na akatambua kuwa Mwenyezi Mungu ndiye atoaye riziki kulingana na jitihada ya mja wake NAJINSI MJA HUYO ANAVYO MTANGULIZA Mola wake katika jitihada hizo, basi bila shaka imani za kishirikina katika suala zima la utafutaji hasa wa mali ingetoweka na ndugu zetu Albino wangepata maisha ya amani na utulivu na hata wazee wetu kule Shinyanga na Simiyu nao pia wangepata tumaini la amani.

Hizi kwa hakika ni baadhi tu ya faida zinazopatikana kwa kuingiza mafundisho ya Qurani tukufu katika maisha yetu ya kila siku. Ni wajibu wa kila Mwanajumuiya kujitahidi kadiri ya awezavyo kuhuisha ari ya usomaji wa Qurani tukufu na kufuata kikamilifu mafundisho yake. Hii itawezekana tu kama kila mmoja wetu na yakini ya kutosha juu ya Mwenyezi Mungu na kuzidi katika ibada na kuomba msaada wa Mwenyezimungu.

# Mwenendo mwema unaotarajiwa kwa kila Ahmadiyya

***Kutoka toleo lililopita***

***Hotuba iliyotolewa kwenye Jalsa Salana 2014 na Sheikh Bakri A. Kaluta***

Akiwanasihi wale wafanyao Baiat, Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema:

"Baada ya kuingia ndani ya Jumuiya hii unapaswa kubadili mwenendo wa maisha yako ili uwe na imani ya kweli ya Mwenyezi Mungu Naye Awe msaidizi wako katika kila msiba. Halafu usiyapuuze maagizo Yake bali uiheshimu kila amri yake na utoe uthibitisho wa heshima hiyo kwa vitendo vyako."

"Kuvielekea vitu vya kidunia kwa sababu mbali mbali na kuvitegemea, na kuacha kumtegemea Mwenyezi Mungu, ni Shirki (Ushirikina), na inakuwa sawa na kumkana Mwenyezi Mungu. Mvichukulie vitu vya kidunia kwa kiasi cha kutomshirikisha Mwenyezi Mungu. Itikadi yetu ni kwamba hatukatazi kunufaika na vitu vya kidunia lakini twakataza kuvitegemea. Mkono wako ufanye kazi wakati moyo wako ukiwa umeambatana na Mpendwa wa Kweli (Mwenyezi Mungu)".

"Tazamaeni nyinyi mliofanya Baiat na kukiri wakati huu, ni rahisi kusema hayo kwa mdomo lakini ni vigumu kuyatekeleza, kwa sababu Shetani hujishughulisha katika juhudi hii kwamba mwanadamu asiijali dini. Humuonyesha kuwa ni rahisi kuipata dunia na manufaa yake na dini kuwa ni kitu cha mbali, kwa namna hii moyo huwa mgumu na hali yake ya baadaye inakuwa mbaya zaidi kuliko ya awali. Kama wataka kumridhisha Mwenyezi Mungu basi weka nguvu na juhudi zako zote katika kuitimiza ahadi hii ya kuepukana na dhambi."

"Msiseme neno lolote la fitna, msieneze shari, fanyeni subira mtukanwapo, msizozane na yeyote, na hata yule anayezozana nanyi mumtendee kwa wema na upole. Onyesheni mfano bora wa maongezi mazuri, tiini kila agizo kwa moyo mkunjufu kiasi ya kwamba Mungu Aridhike na hata adui pia afahamu kwamba mtu huyu baada ya kufanya Baiat amekuwa tofauti na alivyokuwa awali. Toeni ushahidi wa kweli kwenye kesi. Wale waingiao ndani ya silsila hii wanapaswa washikamane na ukweli kwa moyo wote, nguvu zote na roho yote." [Dhikre Habib uk 436 – 438].

Akiendelea kusisitiza, Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema:

"Baiat yenu hii ni Baiat ya toba. Toba ni za aina mbili. Ya kwanza yahusiana na madhambi yaliyopita, yaani kwa ajili ya kuyarekebisha, ayatolee fidia makosa aliyoyafanya hapo awali, na kujitahidi kadiri iwezekanavyo kuyarekebisha makosa hayo na kujiepusha na madhambi yajayo na kujiokoa na moto huu.

Ni ahadi ya Mwenyezi Mungu kwamba madhambi yote yaliyopita husamehewa kutokana na toba kwa sharti hii kwamba toba hiyo iwe kwa moyo wa kweli na nia safi na kusiwe kumejificha ndani ya kona yoyote moyoni aina yoyote ya udanganyifu.

Yeye Huzifahamu siri zilizofichika za nyoyoni. Yeye Hadanganywi na yeyote. Hivyo msijaribu kumdanganya na mtubie Kwake kwa ukweli sio kinafiki. Toba kwa ajili ya mwanadamu sio kitu cha ziada wala kisicho na faida, na athari yake haiishii tu siku ya Kiama bali inamsahihishia mwanadamu masuala yake yote ya kidunia na ya kiimani na hujaaliwa hali njema na utulivu katika dunia hii na huko Akhera. (Malfuudhaat jal. 5 uk. 187 – 188).

Masharti kumi ya Baiati yaliyoorodheshwa na Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s. yanathibitisha ukweli huu.

Sharti la kwanza la Baiat linaagiza kwamba "Mwenye kufanya Baiat aahidi jambo hili kwa moyo wa kweli kwamba atajiepusha na kumshirikisha Mwenyezi Mungu hadi aingiapo kaburini."

Mwenyezi Mungu katika sura An-Nisaa aya ya 49 Anasema:

Tafsiri yake ni hii kwamba kwa yakini Mwenyezi Mungu Hatamsamehe anayemshirikisha na chochote na mbali na hayo Atasamehe kila kitu kwa yule Amtakaye na yule amshirikishaye Mwenyezi Mungu kwa hakika amezua dhambi kubwa.

Kuhusiana na jambo hili Hadhrat Masih Mauu'd a.s anasema:

"Halikadhalika Mwenyezi Mungu Anasema katika Qurani tukufu:- Kila dhambi itasamehewa lakini Mwenyezi Mungu Hatasamehe Shirk, hivyo msiikaribie Shirk na muifahamu hiyo kuwa ni mti ulioharamishwa." (Zamima Tohfa Golarwiya,Ruhani Khazain jal. 17 uk. 323 – 324 Hashiya).

Tena akasema: "Hapa mradi wa Shirk sio tu kuyaabudu mawe n.k. bali hata kuvitegemea kikamilifu vitu vya kidunia na kujiegemeza mno kwenye vile vinavyoabudiwa duniani ni Shirk." (Al Hakam jal.7 No. 21 Trehe 30 June 1903 uk. 11).

Hapa wanajumuika hata wale wanaojiegemeza kwenye imani za kishirikina za kuamini mambo ya uchawi, ulozi, kupandwa na mashetani na majini, kuchukuliwa misukule n.k. kwani itikadi na mielekeo ya aina hii humrudisha mtu nyuma kabisa katika maendeleo ya kidini na kidunia.

Sharti la pili la Baiat linasema: "Kwamba atadumu kujiepusha na uongo, zinaa, kutazama vilivyokatazwa, kila uovu, dhulma, hiyana, ufisadi na uasi na hatashindwa kujizuia na tamaa mbaya za nafsi yake hata kama ashikwe na jadhba kiasi gani."

Mwenyezi Mungu Anasema ndani ya Kurani Tukufu:
Na tafsiri yake ni hii: Yeyote avitukuzaye vitu vile ambavyo Mwenyezi Mungu Amevifanya kuwa vitakatifu basi hiyo ni heri kwake mbele ya Mola wake na mmehalalishiwa wanyama isipokuwa wale mnaotajiwa, basi jiepusheni na uchafu wa masanamu na mjiepushe kusema uongo. [Al Hajj : 31]. Hapa, uongo pia umewekwa pamoja na shirk.
kuna hadithi moja ya Imam Ahmad bin Hanbal isemayo: "Hadhrat Abu Huraira(r.a) anasimulia ya kwamba Mtume (S.A.W) alisema mtu aliye mwita mtoto mdogo na kumwambia njoo hapa nikupe kitu na asimpe basi hiyo itahesabiwa kuwa ni uwongo." (Musnad Ahmad bin Hanbal Jd.2 Uk. 452 chapa ya BEIRUT.)
Akiifafanua Hadithi hii, Hadhrat Khalifatul Masih V atba anasema:
"Jambo hili ni muhimu sana kwa ajili ya Tarbiat au malezi bora. Angalieni, katika malezi ya watoto, kusiwe na jambo hili hata katika sura ya utani. Waila namna hiyo hiyo katika hiyo hiyo njia ya utani, watoto huanza kujenga tabia ya kusema kisicho sahihi, ambapo baadae hali hii inapokomaa anakuwa haoni kasoro yoyote katika kusema uongo na hata hisia zake juu ya jambo hili hutoweka."
Hadhrat Masih Mau'ud (a.s) anasema, " Kurani Tukufu imesema kuwa uwongo pia ni najisi na ni uchafu uchukizao, kama vile ilivyosema: -

(SURA AL- HAJI – Aya 31) [Tafsiri: - 22:31 – Jiepusheni na uchafu wa masanamu jiepusheni na usemi wa uwongo.]
Tazameni, hapa uongo umewekwa mkabala na sanamu na kwa hakika hata uongo ni sanamu, waila kwa nini mtu aache ukweli na aelekee upande mwingine (wa uwongo)? Kama vile ambavyo hakuna uhakika wowote ule katika sanamu, halikadhalika chini ya uongo hakuna chochote zaidi ya unafik tu.

Waongo wanakuwa hawaaminiki kiasi ya kwamba hata kama waseme ukweli hufikiriwa tu lazima katika kauli yao kuna mchanganyiko wa uwongo. Ikiwa wasemao uwongo watapenda kupunguza kusema uwongo haitawezekana kuondokana nao kwa haraka, ni baada tu ya kujizoeza kwa muda mrefu ndipo watakapokuwa na tabia ya kusema kweli." (Malfuuzaat Jld. 3 Uk. 350).

SHARTI LA TATU LA BAIAT
Atadumu kusimamisha sala tano, bila kukosa, sawa na hukumu ya Mwenyezi Mungu na Mtume(S.A.W). Na atadumu, kadiri awezavyo, kusali sala ya tahajjud, kumsalia Mtume wake mtukufu s.a.w., kuomba msamaha wa dhambi zake kila siku na kufanya istighfar. Na kwa dhati ya moyo atazikumbuka hisani za Mwenyezi Mungu na kumhimidia na kumsifu kila siku.

SHARTI LA NNE LA BAIAT
"Ya kwamba hatawadhuru, kwa Ujumla viumbe vyote vya Mwenyezi Mungu, na hususan Waislamu, kwa sababu ya tamaa mbaya ya nafsi yake, si kwa mkono wake, wala kwa ulimi na viungo vyake vingine."
SHARTI LA TANO LA BAIAT
Atakuwa radhi juu ya kudra ya Mwenyezi Mungu katika kila hali ya taabu na raha, dhiki na faraja, msiba na neema. Kwa neno zima atakuwa tayari kukubali fedheha na maumivu katika njia ya Mwenyezi Mungu. Naye atakapopata msiba wowote hatageuka nyuma bali ataendelea mbele kufuata na kutii amri yake Mungu.

SHARTI LA SITA LA BAIAT
Atajiepusha kufuata mila za watu na matamanio mabaya ya nafsi na atajisalimisha kikamilifu kwenye utawala wa Kurani Tukufu na mwenendo wake katika kila njia siku zote utawiana na kauli ya Mwenyezi Mungu na kauli ya Mtume s.a.w.

SHARTI LA SABA LA BAIAT
"Ataacha kabisa kufanya kiburi na majivuno na ataishi kwa tabia njema na huruma na atakaa kwa unyenyekevu, kwa adabu na upole sana."

SHARTI LA NANE LA BAIAT

"Atafahamu dini na heshima yake na kazi ya Uislamu kuwa ni bora kuliko mali yake na heshima ya nafsi yake na kuliko watoto wake na wapenzi wake wote wote."

SHARTI LA TISA LA BAIAT
Atawahurumia daima viumbe vya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu; sawa na uwezo wake naye atawaneemesha kwa zile neema alizopewa yeye na Mwenyezi Mungu.

SHARTI LA KUMI LA BAIAT
Katika ahadi hii ya udugu, atakayofungamana nami kwa sharti ya kutii kila amri njema, atatimiza ahadi hii mpaka kufa kwake na katika ahadi hii ya undugu ataonyesha utii na unyenyekevu wake kwa imara zaidi kuliko ufungamano wowote wa damu au wa bwana na mtumishi.

# Baraka za Ukhalifa katika zama hizi

***Kutoka toleo lililopita***

***Hotuba iliyotolewa kwenye Jalsa Salana 2014 na Sheikh Waseem Ahmad Khan***

Tena mapinduzi haya haya yanaendelea kujitokeza huko Urusi, ushuhuda wake ndio mamia ya barua zitokazo huko kwenda kwa Khalifa Mtukufu ziandikwazo na wanaajumuiya warusi na majibu yapatikanapo watu hao wanazibusu barua za Khalifa na wengine wanazitunza katika fremu na kuziweka nyumbani mwao.

Ndugu wasikilizaji, kazi kubwa na yenye kuleta mabadiliko makubwa duniani ifanyikayo katika zama za leo iliyofungua milango mipya kwa ajili ya Jumuiya ni hii kwamba Khalifa Mtukufu alialikwa kutoa hutuba katika bunge kubwa la dunia ambapo Allah Subhanahu wa Taala Alimjaalia khalifa wake kutoa hutuba juu ya mafundisho bora ya Islam.

Katika bunge la Marekani, bunge la Umoja wa Ulaya, bunge la Uingireza, bunge la Newzealand, katika makao makuu ya kijeshi ya Ujerumani, nchi za Singapore, Australia, Japan, Canada na nchi zingine nyingi za Ulaya mikutano ilifanyika, katika mikutano hiyo mawaziri, wabunge, wabalozi, maafisa wa kijeshi, maafisa wa ulinzi, wakurugenzi wa idara mbalimbali, mameya, madiwani, wakuu wa vyuo, madaktari, mawakili, wahandisi, waandishi wa habari na wanasiasa walishiriki. Khalifa Mtukufu kwa kuwakilisha Islam aliweza kuweka mbele yao mafundisho ya Islam na kuwashawishi wachangie mchango wao mzuri katika kuleta amani duniani.

Ndugu waahmadiyya, leo wapinzani wa Islam huonesha Islam kuwa ni dini ya ugaidi tu na vyombo vya habari vya magharibi vipo mbele katika mpango huu, Khalifa wetu Mtukufu kwa kutoa hutuba mbalimbali, kuonana na viongozi tofauti pamoja na kutoa maagizo kwa viongozi wa jumuiya nao pia wajishughulishe katika hilo anaondoa na kufutilia mbali madoa haya yote, basi hayo ni yale maendeleo na mafanikio yapatikanayo duniani kwa kupitia Ukhalifa, leo viongozi wa dunia wanakuja kwa khalifa kuomba ushauri wake na kupata maombi yake kwani nao pia wanaelewa kuwa amani, usalama na ukombozi wa kweli wa dunia umeunganishwa na Ukhalifa.

Ndugu wapendwa ili neema hii ibaki pamoja nasi milele, basi jukumu letu la kwanza ni kuonesha utii wa hali ya juu na hicho ndicho kitu kitakachotuunganisha sisi na Ukhalifa, utii uoneshwao na mfuasi wa Masihi Maaud Hadhrat khalifa tul Masih awwal Hakim Molvi Nurudin ra.

Seyydna Ahmad as alisema

Ingependezaje kama kila mtu wa jumuiya angekuwa ni Nurudin, lakini hii yawezekana tu kama kila moyo ujae nuru ya yakini.

Hadhrat Khalifa tul Masih wa nne ra alisema, neema hii mmeipata baada ya karne kumi na tatu, muipende na kuienzi zaidi kuliko nafsi zenu. Funguo zote za usalama na uhai wenu zimewekwa katika nidhamu ya Ukhalifa, uhai wa umma wa kiislam umo katika kujiunga na Ukhalifa, fanyeni ahadi ya kuilinda neema hiyo kwa kusema kama walivyosema Maansar wa Madina ya kwamba, Ewe Khalifa wetu hatutasema kama walivyosema watu wa Musa kwamba nenda wewe na Mola wako mkapigane, bali sisi tutapigana kulia kwako na kushoto kwako mbele yako na nyuma yako na adui hataweza kukufikia mpaka akanyage juu ya maiti zetu.

Hadhrat khalifa tul Masih wa Tano a.h.t kwa kutunasihi sisi wapokeaji wa neema ya Ukhalifa alisema, huu ni mpango wa Allah na ahadi yake Ambaye kamwe Hafanyii ahadi ya uongo ya kwamba wapendwa wa Masihi Maaud as ambao kutokana na kufuata amri yake wamejiunga na kudra ya pili watashinda duniani, kwani Mungu Yupo pamoja nao, Mungu yupo pamoja nasi.

Leo ni wajibu wa wanajumuiya wote kujitahidi kutimiza shabaha ya kufika kwa Hadhrat Ahmad as, tunalo jukumu la kuwaleta Wakristo, Mayahudi, Mabaniani na wafuasi wa dini zote chini ya bendera tukufu ya mtume Muhammad saw, huu ni ukhalifa wa kiahmadiyya utakaokusanya waislamu wote, fikisheni ujumbe huu kwa kila mwenzenu ya kuwa ukombozi wenu wa hakika umo katika kumtambua Imam wa zama kwani huyu ndiye mdhamini mkweli wa amani na usalama, basi njooni jiungeni na jumuiya yenye imamu mmoja na tekelezeni amri ya Bwana wetu mtukufu Muhammad saw isemayo

Mushikamane na Jumuiya ya Waislamu itakayokuwa na Imamu mmoja atakayekuwa Khalifa wa Allah na msipofanya hayo basi kumbukeni ya kuwa mwisho wenu utakuwa mbaya, kifo chenu kitakuwa cha ujinga kwani Mtume wangu mtukufu saw alisema, atakayekufa ilhali hakumtambua imamu wake basi amekufa kifo cha ujinga.

Allah Atusaidie kutekeleza wajibu wetu. aamin

# Mkoa wa Shinyanga wapata Mapinduzi Makubwa

## *Jalsa salana ya Mkoa yafanyika kwa mafanikio*

***Na Mwandishi Wetu***

Ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. unaendelea kudhihirika kila siku kama alivyoahidiwa na Mwenyezi Mungu kwamba: Hakika Mimi nitafikisha ujumbe wako katika kila pembe ya dunia.

Hicho ndicho kinachotokea kwenye mkoa wa Shinyanga kwa sasa. Shinyanga ni Mkoa unaoonekana na wengi kwamba ni miongoni mwa mikoa iliyo na wapagani (watu wasioamini dini yoyote) wengi zaidi kuliko mikoa mingine mingi ya Tanzania.

Shinyanga ni mkoa ambao umegubikwa na mauaji mengi hasa ya vikongwe yakinasibishwa na imani za uchawi ambazo wakazi wengi wa mkoa huo wanazo.

Pamoja na hali hiyo iliyodhaniwa kuwa ni kame, kwa msaada wa Mwenyezi Mungu hivi karibuni Jumuiya imaenza zoezi la mahubiri ya nguvu kwenye eneo hilo na kwa fadhili za Mwenyezi Mungu juhudi hizo zimeanza kuzaa matunda, kwa ndugu wengi kuukubali ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa na kujiunga nao. Miongoni mwa vijiji ambavyo viliitikia wito huo mwanzoni ni kijiji cha Sungamile kilichopo kilomita chache kuelekea Makao Makuu ya Wilaya ya Kahama. Vijiji vingine ni pamoja na Tinde, Nsalala na Kidanda.

Pamoja na upinzani mkubwa ulioletwa na wale wasiotafakari vizuri wakati haki iwafikiapo na hivyo kupelekea walimu wetu na baadhi ya wanajumuiya kupata shida na usumbufu wa aina moja au nyingine, ndugu hawa waliojiunga wamebaki kuwa imara na wenye jazba juu ya imani yao.



***Sehemu ya waumini wa Jumuiya (Waahmadiyya Wapya) katika kijiji cha Sungamile wakimpokea kwa salamu Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry wakati alipotembelea tawini hapo kwa ajili ya ufunguzi wa msikiti***

Wapinzani wamejaribu kutumia kila mbinu lakini wameshindwa na wakati mwingine wamefedheheka sawa na ahadi ya Mwenyezi Mungu aliyompa Masihi Aliyeahidiwa kwamba: "Mimi nitamfedhehesha kila atakayetaka kukufedhehesha wewe."

Akiwa safarini kutemebelea mikoa ya Mwanza na Shinyanga hivi karibuni , Amir na Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry aliyatembelea matawi hayo mapya na kuongea na wanajumuiya katika kuwakumbusha wajibu na makusudio ya kujiunga kwao na Jumuiya.

Aidha akiwa kijijini Sungamile, alifungua msikiti na nyumba ya Mwalimu ambayo imejengwa hivi karibuni katika kijiji hicho.

Miongoni mwa mafanikio makubwa na ya kihistoria yaliyopatikana mkoani Shinyanga ni pmaoja na kufanyika kwa Jalsa Salana kwa mara ya kwanza katika Mkoa huo. Jalsa salana hiyo ilifanyika siku ya tarehe 20/11/2014 katika mji mdogo wa Tinde na ilikuwa na mahudhurio mazuri ya wanajumuiya zaidi ya 600.

Miongoni mwa mambo ya kusisimua yaliyotokea kwenye eneo hili ni kunyesha kwa mvua kubwa na ya ghafla mara tu baada ya kumalizikja kwa Jalsa hiyo ambapo na sawa na walioishuhudia mvua hiyo walisema iliashiria baraka kwani ilinyesha kwenye eneo la mji huo mdogo tu wakati maeneo ya jirani ya kilomita chache tu kila upande hakukuwa na hata tone la mvua.

Tukio jingine la kusisimua ni pale wapinzani walipoondoka kwa fadhaa siku ya pili baada ya Jalsa na kuwaendea wakazi wa kijiji cha jirani cha Nsalala na kuwaongopea kwamba (Mungu apishe mbali) eti "Waahmadiyya ni Freemasonry na wamekulisheni nyama ya binadamu kwenye mkutano wa jana kule Tinde". Kwa mshangao wakazi hao waliwaeleza kwamba ni kweli leo tumethibitisha uongo wenu kwani nyama iliyotumika kwenye hafla hiyo ilichinjwa na sisi wenyewe, mnyama tulimnunua sisi wenyewe na wapishi tulikuwa sisi wenyewe na hakuna hata Ahmadiyya mmoja mkongwe ambaye alifika jikoni hata kuchungulia bali sisi ndio tuliowagawia chakula. Wapinzani hao wakaondoka kichwa chini kwa aibu.

Kwa ajili ya malezi ya wanajumuiya hao wapya, tayari Amir na Mbashiri Mkuu ameshatangaza mpango wa malezi kwa kipindi cha mwaka nzima na pia ameutangaza mwaka 2015 kuwa ni mwaka wa Tabligh katika mikoa ya Shinyanga na Mwanza.

Amir Sahib amewaomba wanajumuiya wote washiriki kwa njia moja au nyingine katika mpango huu wa Tabligh na Tarbiyyat ili wanajumuiya hao wapya waweze kulelewa na wasije wakarudi nyuma kama ilivyowahi kutokezea kwa vijiji vingine miaka ya nyuma.

Mwenyezi Mungu Awasaidie sana ndugu hawa wapya na awaongoze wakazi wa mkoa wa Shinyanga kwenye njia yake iliyoonyooka. Amin.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

# MapenziyaMungu

Rab. 1/ Rab. 2. 1436 AH | Januari 2015 | Sulhu 1394 HS

**Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w**

Imesimuliwa na Hadhrat Ibn Umar r.a. ya kwamba mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Mwislamu ni nduguye Mwislamu mwenzake, hamdhulumu wala hamwachi bila msaada. Amtimiziaye haja nduguye, Mungu Atamtimizia haja yake. Amwondoleaye Mwislamu shida, Mungu Atamwondolea shida miongoni mwa shida za siku ya Kiyama na amsitiriye Mwislamu, Mungu Atamsitiri siku ya Kiyama. *(Bukhari).*

## KALENDA: 2015 AD, 1436 - 1437 AH, 1394 HS

| January | | Sulhu | | Raby'al-awal - Raby'al-Thaany | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mon | Tue | Wed | Thu | Fri | Sat | Sun |
| | | | 1 | 2 | 3 | 4 |
| 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 |
| 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 |
| 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 |
| 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | 31 | |

| February | | Tabligh | | Raby'al-Thaany - Jumaada al-awal | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mon | Tue | Wed | Thu | Fri | Sat | Sun |
| | | | | | | 1 |
| 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |
| 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
| 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 |
| 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | |

20 - Siku ya Mwana Aliyeahidiwa

| March | | Amman | | Jumaada al-awal - Jumaada al-Thaany | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mon | Tue | Wed | Thu | Fri | Sat | Sun |
| 30 | 31 | | | | | 1 |
| 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |
| 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
| 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 |
| 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 |

23 - Siku ya Masihi Aliyeahidiwa

| April | | Shahadat | | Jumaada al-Thaany - Rajab | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mon | Tue | Wed | Thu | Fri | Sat | Sun |
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 |
| 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 |
| 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 |
| 27 | 28 | 29 | 30 | | | |

25 - 26 Shura ya Kitaifa

| May | | Hijrat | | Rajab - Sha'baan | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mon | Tue | Wed | Thu | Fri | Sat | Sun |
| | | | | 1 | 2 | 3 |
| 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
| 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 |
| 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 |
| 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | 31 |

27 - Siku ya Ukhalifa

| June | | Ihsan | | Sha'baan - Ramadhaan | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mon | Tue | Wed | Thu | Fri | Sat | Sun |
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
| 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 |
| 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 |
| 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 |
| 29 | 30 | | | | | |

12-14 Khuddam Ijtimaa | 12-14 Lajna Ijtimaa | 18 Ramadhan

| July | | Wafa | | Ramadhaan - Shawwal | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mon | Tue | Wed | Thu | Fri | Sat | Sun |
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 |
| 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 |
| 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 |
| 27 | 28 | 29 | 30 | 31 | | |

18 - Eid ul Fitri

| August | | Zahoor | | Shawwal - Dhul-Qa'dah | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mon | Tue | Wed | Thu | Fri | Sat | Sun |
| 31 | | | | | 1 | 2 |
| 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 |
| 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 |
| 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 |
| 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |

| September | | Ikha | | Dhul-Qa'dah - Dhul-Hijjah | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mon | Tue | Wed | Thu | Fri | Sat | Sun |
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |
| 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 |
| 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 |
| 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 |
| 28 | 29 | 30 | | | | |

18 - 20 Jalsa Salana Tanzania | 24 - Eidul Adh'ha

| October | | Tabook | | Dhul-Hijjah - Muharram | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mon | Tue | Wed | Thu | Fri | Sat | Sun |
| | | | 1 | 2 | 3 | 4 |
| 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 |
| 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 |
| 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 |
| 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | 31 | |

| November | | Nubuw-wat | | Muharram - Safar | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mon | Tue | Wed | Thu | Fri | Sat | Sun |
| 30 | | | | | | 1 |
| 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 |
| 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
| 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 |
| 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 |

| December | | Fatah | | Safar - Raby'al-awal | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mon | Tue | Wed | Thu | Fri | Sat | Sun |
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |
| 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 |
| 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 |
| 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 |
| 28 | 29 | 30 | 31 | | | |

12 - 13 Ansarullah Ijtimaa

*Zingatia: Kuanza kwa Ramadhani, na Idi zote mbili kunategemea mwandamo wa mwezi*